# MADA

# MOFOSINTAKSIA YA KISHAZI NOMINO CHA KISWAHILI SANIFU: MTAZAMO WA UMINIMALISTI

Na

NOREEN MBESA MWALILI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

IDARA YA ISIMU NA LUGHA

JULAI, 2008

University of NAIROBI Library
0472979 4

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

______________________________ 5.11.2008
NOREEN MBESA MWALILI TAREHE
(MWANAFUNZI)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi.

______________________________ 7th November 2008
PROF. ABDULAZIZ M.H. TAREHE
(MSIMAMIZI)

______________________________ 5.11.2008
DKT. HELGA SCHROEDER TAREHE
(MSIMAMIZI)

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa:

**Virginia M. Mwalili**

Na

**Patrick H. Mwalili**

## SHUKRANI

Waloamba waliamba na kweli nimekuja kuamini hakuna ajiwezaye. Isingekuwa ni usaidizi wa wengi, nitakaowataja na wengine ambao sitawataja, hakika kozi hii ingeniwia ngumu sana. Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwenu nyote mlionishika mkono katika safari hii, mkanihimiza na kunitia moyo kila hatua.

Kwanza kabisa, ningependa kumshukuru Manani kwa kunipa sio uhai na siha tu, bali pia fursa hii ya kuutalii uwanja ambao ingawa wengi wametamani, hawajajaliwa. Hakika kuota ni jambo afanyalo kila binadamu kwa hiari ama bila hiari lakini fursa ya kutekeleza ndoto hupangwa na Mola. Asante kwa kunifungulia njia ya kuitekeleza ndoto yangu inayotimia miaka kumi sasa.

Pili, natoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu, Profesa Abdulaziz M. H. Na Dkt. Helga Schroeder kwa kunisimamia, kuniongoza na kunielekeza kwa moyo mkunjufu. Nimefahamu fika kwamba njia ya kufahamu hakika haina kikomo. Shukrani zangu pia nazitoa kwa wahadhiri wengine walionisaidia na kunifaidi kwa njia mbalimbali: Profesa Kithaka wa Mbeeria, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Wamitila, Dkt. Alfred Buregeya, Dkt. Tom Olali, Dkt. John Habwe, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Mutiga, Dkt. Mwenda Mbatiah, Bw. Ayub Mukhwana na Bi. Prisca Jerono.

Wenzangu tuliong'oa nanga pamoja nawashukuru kwanza kabisa kwa kuja kuwajua na kufanya urafiki nanyi. Zaidi ni kwa usaidizi wenu na njia yenu spesheli ya kumwondolea mtu wasiwasi hasa mambo yalipopamba moto: Reuben Kisiroche, Miriam Makanga,

Kenneth Nyaosi, Nyamai, Mheshimiwa Tola Kofa na wanafunzi wote wa Isimu. Betty Karimi kwako wewe shukrani zangu hazina kipimo, hasa kwa urafiki wako na usaidizi wako katika maji haya tuliyoyavulia pamoja. Siwezi kukusahau mwenzangu Silvano Mureithi kwa wema na ukarimu wako. Licha ya kazi nyingi iliyokusonga, ulichukua muda wako kunifafanulia yaliyonishinda tena kwa kina. Asante sana.

Kunao wengine walionifaa na siwezi kukosa kuwataja hapa. Bw. na Bi. Musembi, kwa msukumo mnipao kila uchao na urafiki wenu wa dhati. Willy Muange, sijui ni majaaliwa ama ni nini lakini safari zetu pamoja hunipa moyo kwani twakujua tutokako. Dadangu mpendwa, Sarah Mbithe, sijui ningefanya nini bila wewe. Wazazi wangu, kwa kuuhisi uwepo wenu maishani mwangu kila siku, kila hatua. Mwishowe ni kwa mabinti zangu, Lydia Ndindi na Cynthia Mbula, kwa kuwa wanangu, kwa uvuumilvu wenu, usaidizi wenu, mapenzi yenu na juu ya yote kwa ari mnipayo kila niwaonapo na kuwafikiria.

# ORODHA YA VIFUPISHO

ak – athari ya kiima

akij – athari ya kijalizo

at – athari ya kitenzi

ats - athari ya kitenzi kisaidizi

atk - athari ya kitenzi kikuu

ay – athari ya yambwa

DH - Dhamira

H – Hali

JLZ – Kijalizi

KALea - Kauli ya Kutendea

KALesh – Kauli ya Kutendesha

KAL ewa – Kauli ya Kutendewa

KALik - Kauli ya Kutendeka

KAN – Ukanusho

KE – Kirai Elezi

KH – Kirai Husishi

KN – Kirai Nomino

KT – Kirai Tenzi

KV – Kirai Vumishi

KSU – Kitenzi Kisoukomo

khj - kama hapo juu

Kij – Kijalizo

KUPk – Kirai Upatanisho wa Kiima

KUPkij – Kirai Upatanisho wa Kijalizo

KUPy – Kirai Upatanisho wa yambwa

NJ – Njeo

n.k. - na kadhalika

Spes – Spesifaya

SZGM - Sarufi zalishi Geuza Maumbo

T.Y. - Tafsiri Yetu

T - Kitenzi

UF - Umbo Fonetiki

UM - Umbo Mantiki

U&M - Umilikifu na Masharti

UP - Upatanisho

UPk – Upatanisho wa Kiima

UPy – Upatanisho wa Yambwa

UPkij - Upatanisho wa Kijalizo

UPrej - Upatanisho wa Kirejeshi

Ø – mofu kapa

*xyz - si sahihi

xyz* - tazama ufafanuzi hapo chini

⟶ - hubadilika kuwa

{ } - mipaka ya mofimu

# TAFSIRI ZA DHANA ZILIZOTUMIWA

Athari - Trace

Gongana - Crash

Kanuni ya iktisadi - Economy Principle

Kanuni ya kucheleshwa - Principle of Procrastination

Kanuni ya usogezi mfupi - Principle of shortest move

Kanuni ya ubinafsi - Principle of Greed

Kanuni ya ufafanuzi wa Kina - Principle of full interpretation

Kifundo - Node

Kijalizo - Complement

Kijalizi - Complementizer

Kishazi kikuu - Main clause

Kishazi bebwa - Embedded clause

Kishazi jalizi - Complement clause

Kishazi tegemezi - Dependent clause

Kishazi kisoukomo - Infinitive clause

Kitita cha sifa dhahania - Bundle of abstract features

Kukutana - Converge

Kuungana - Merge

Kirai kipatanishi yambwa - Phrasal agreement object

Kirai kipatanishi kiima - Phrasal agreement subject

Leksikoni - Lexicon

Mdhihirisho wazi - Spell-out

Mifanyiko ya kimkokotoo - Computational processes

Mjumuiko - Interface

Mtenda - Agent

Mtendewa - Benefactor

Mtendwa - Theme

Mrejelewa - Patient

Mwathiriwa - Experiencer

Nadharia ya ukaguzi wa sifa - Feature- checking theory

Nadharia ya ukaguzi wa uhusika -Case checking theory

Nomino hisivu - Animate noun

Numerali - Numeration

Sarufi bia - Universal grammar

Spesifaya - Specifier

Uambatani - Coordination

Utegemezi - Subordination

Usogezi - Movement

Umbo fonetiki - Phonetic form

Umbo Mantiki - Logic form

Umilisi - Competence

Utendaji - Perfomance

Upatanisho dhaifu - Weak agreement

Upatanisho thabiti - Strong agreement

Ujenzi miundo - Structure building

Uvurumishaji - Projection

Wasilisho - Representation

# MUHTASARI

Utafiti huu ni jaribio la kuchanganua kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu. Kishazi nomino ni kishazi tegemezi ambacho huelekea kuchukua majukumu ya kirai nomino katika sentensi.

Kazi hii imegawika katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa kazi yenyewe. Katika utangulizi huu tumeelezea sababu zetu za kuchagua mada na kuorodhesha madhumuni ya utafiti huu. Isitoshe, tumeufafanua msingi wa nadharia tuliyotumia na kupitia yaliyoandikiwa kuhusu mada tunayoishughulikia. Katika sura ya pili, tumetoa muhtasari wa maelezo ya dhana za kisarufi tunazoshughulikia kwa njia moja au nyingine. Katika sura ya tatu, tumeainisha kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu katika kategoria tatu na tukatoa ufafanuzi wake. Pia tumezitathmini nafasi za kisarufi zinazochukuliwa na kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu. Sura ya nne imeshughulikia upatanisho wa kisarufi wa kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu na kishazi kikuu na sura ya tano ni hitimisho ambapo tumeelezea tuliyoyatambua na kutoa mapendekezo.

# YALIYOMO

Mada ........ i

Ungamo ........ ii

Tabaruku ........ iii

Shukrani ........ iv

Orodha ya vifupisho na ishara ........ vi

Tafsiri ya dhana zilizotumiwa ........ viii

Muhtasari ........ x

**1. SURA YA KWANZA:**

1.0 Utangulizi ........ 1

1.1 Mada ya utafiti ........ 3

1.2 Madhumuni ya utafiti ........ 4

1.3 Nadharia tete ........ 4

1.4 Sababu za kuchagua mada ........ 5

1.5 Upeo na mipaka ........ 6

1.6 Msingi wa nadharia ........ 7

1.6.1 Mifanyiko ya kimkokotoo ........ 9

1.6.2 Mofolojia na uminimalisti ........ 12

1.6.3 Kanuni ya ukaguzi sifa ........ 13

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........ 16

1.8 Mbinu za utafiti ........ 22

1.9 Umuhimu wa Utafiti ........ 23

**2. SURA YA PILI: SENTENSI NA VIPASHIO VYAKE**

2.0 Utangulizi ........ 24

2.1 Dhana ya sentensi ........ 24

2.2 Vipashio vya sentensi ........ 26

2.2.1 Maneno ........ 27

2.2.2 Virai ........ 43

2.2.3 Vishazi ........ 47

2.3 Aina za sentensi ........................................ 49
2.4 Hitimisho ........................................ 53

**3. SURA YA TATU: KISHAZI NOMINO CHA KISWAHILI SANIFU**
3.0 Utangulizi ........................................ 54
3.1 Kishazi Nomino ........................................ 54
3.1.1 Kishazi Nomino Rejeshi ........................................ 55
3.1.2 Kishazi Nomino Kisoukomo ........................................ 57
3.1.3 Kishazi Nomino Kwamba ........................................ 58
3.2 Nafasi za Agiumenti ........................................ 60
3.3 Vishazi nomino vya Kiswahili sanifu katika nafasi za agiumenti ........................................ 63
3.3.1 Mtenda ........................................ 64
3.3.2 Mtendwa ........................................ 67
3.3.3 Mwathiriwa ........................................ 69
3.3.4 Mrejelewa ........................................ 70
3.3.5 Mtendewa ........................................ 71
3.4 Vishazi nomino vya Kiswahili sanifu katika nafasi zisizo za agiumenti ........................................ 73
3.4.1 Kiima ........................................ 74
3.4.2 Kijalizo cha kiima ........................................ 76
3.4.3 Kijalizo cha kivumishi ........................................ 78
3.4.4 Kijalizo cha kihusishi ........................................ 81
3.4.5 Kijalizo cha jina ........................................ 82
3.5 Hitimisho ........................................ 84

**4. SURA YA NNE: RUWAZA YA UPATANISHO WA KISHAZI NOMINO**
4.0 Utangulizi ........................................ 85
4.1 Ruwaza ya upatanisho katika Kiswahili sanifu ........................................ 85
4.2 Upatanisho wa Kishazi Nomino Rejeshi ........................................ 88
4.3 Upatanisho wa Kishazi Nomino Kisoukomo ........................................ 94
4.4 Upatanisho wa Kishazi Nomino Kwamba ........................................ 97

4.5 Hitimisho .......... 102

5. SURA YA TANO: HITIMISHO

5.0 Hitimisho .......... 103

5.1 Mapendekezo .......... 105

Marejeleo .......... 107

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kibantu inayozungumzwa Afrika Mashariki na baadhi ya sehemu za Afrika ya kati. Lugha hii ilianza kusanifishwa chini ya utawala wa mkoloni kwa malengo ya kutaka lugha hii itumiwe kuwafundishia Waafrika shuleni. Lahaja ya Kiunguja ilichaguliwa kama msingi wa kuisanifisha lugha na lahaja nyingine zikachangia. Othografia iliyotumiwa iliboreshwa, kamusi na vitabu vikaandikwa. Hivi sasa, lugha ya Kiswahili inazidi kukua na kupanuka na ndiyo sababu tunaona haja ya kufanya utafiti wetu katika lugha hii kwani tunafahamu kuwa utafiti wa lugha husaidia katika kuikuza lugha.

Kipashio kikubwa kabisa katika sintaksia ni sentensi. Wanasarufi wa kimapokeo walielezea sentensi kama kipashio kikuu/huru cha kisintaksia ambacho hakiwezi kuegemezwa katika muundo mwingine wa kisintaksia kwa kutumia kanuni yoyote ya kisarufi. Sentensi ni kipashio cha kisarufi kinachoundwa kwa vipashio vidogo kuanzia mofimu, neno, kirai na kishazi. Mofimu huungana pamoja kuunda neno. Maneno nayo huungana pamoja kuunda virai ambavyo huungana kuunda vishazi. Sentensi huweza kuundwa kwa kuunganisha virai mbalimbali ama vishazi vya hadhi sawa ama tofauti. Kishazi ni kipashio cha kisarufi ambacho ni kidogo kuliko sentensi lakini ni kikubwa kuliko kirai. Vishazi vyaweza kuainishwa kwa njia tatu (Leech na Svartik 2000:245):

i) Kwa misingi ya vipashio vinavyokijenga kishazi chenyewe kama vile kiima, kitenzi, yambwa n.k. na ruwaza ya kitenzi kinachoundwa kutokana na vipashio hivi.

ii) Kwa misingi ya vishazi ukomo, vishazi visoukomo na vishazi visivyo na kitenzi.

iii) Kwa misingi ya uamilifu wa kishazi yaani uamilifu wa kishazi katika sentensi. (TY).

Tumevishughulikia vishazi vinavyoainishwa kwa misingi ya uamilifu wake katika sentensi. Vishazi tegemezi vyaweza kuwa na uamilifu mbalimbali katika sentensi. Kwa mujibu wa Quirk na wenzake (1972:731), vishazi tegemezi vina uamilifu wa kiima, yambwa, kijalizo ama kielezi katika sentensi. Katika misingi ya uamilifu, vishazi vyaweza kuainishwa katika kategoria zifuatazo:

i) vishazi nomino

ii) vishazi rejeshi (vishazi vumishi)

iii) vishazi linganishi

iv) vishazi elezi (Leech na Svartik 2000:251)

Vishazi nomino, ambavyo ndivyo tumevishughulikia katika utafiti huu, ni vishazi ambavyo vina uamilifu wa kirai nomino. Kwa mfano:

1. **Aliyetumwa jana** ni mzuri.

Katika sentensi hii, maneno yaliyokolezwa rangi ni kishazi nomino na yanaweza kuondolewa katika nafasi hiyo na ikachukuliwa na nomino kama ilivyo katika mfano huu,

2. **Juma** ni mzuri.

Utafiti huu umechunguza kishazi nomino katika Kiswahili Sanifu.

## 1.1 MADA YA UTAFITI

Kiswahili ikiwa ni lugha ambishibainishi, mofolojia yake huhusiana kwa karibu sana na sintaksia yake. Upatanishi katika Kiswahili ndio unaoathiriwa sana na sifa hii ya lugha ya Kiswahili. Sifa hii, ya kuwa lugha ambishibainishi, ndiyo iliyotutia azma kuchunguza uhusiano wa kimofosintaksia baina ya kishazi nomino cha Kiswahili sanifu na kishazi kikuu. Uchunguzi huu tumeufanya katika mtazamo wa uminimalisti kwa sababu mtazamo huu una sifa ya kujumuisha mofolojia na sintaksia pamoja. Hivyo, katika utafiti huu tumechunguza kama kuna upatanisho wa kisarufi katika kitenzi cha kishazi nomino na kitenzi cha kishazi kikuu.

Mada hii ya utafiti pia, imejumuisha uchunguzi wa uamilifu wa kishazi nomino katika uundaji wa sentensi changamano za Kiswahili Sanifu. Biber na wenzake (1999) wanasema kuwa "kishazi ni kipashio kilichoundwa ndani ya kirai tenzi"(TY). Kama kuendeleza mawazo haya, nadharia ya uminimalisti inadai kuwa kategoria zote amilifu hupatikana katika kirai tenzi. Nadharia hii pia inadai kuwa, ukaguzi hufanywa kwa nia ya kuthibitisha usarufi. Kirai nomino hukaguliwa dhidi ya nafasi za spesifaya za ama upatanisho wa kiima au upatanisho wa yambwa. Tutapendelea kuona kama vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu vimezichukua nafasi hizi za kirai nomino.

Kwa hivyo, utafiti wetu umeongozwa na maswali yafuatayo:

i) Je, kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu kina uamilifu sawa na wa kirai nomino?

ii) Je, kuna upatanisho wowote baina ya kitenzi cha kishazi kikuu na kishazi nomino? Kama upo, ni kipashio gani kinachosababisha upatanisho huu?

iii) Je, kanuni ya ukaguzi sifa katika nadharia ya uminimalisti inafaa katika uchunguzi wa uamilifu wa kishazi nomino katika sentensi changamano za Kiswahili Sanifu?

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika utafiti huu tumenuia:

i) Kubainisha kategoria za vishazi nomino vya Kiswahili sanifu.

ii) Kubainisha kategoria amilifu zinazochukuliwa na kishazi nomino katika sentensi changamano.

iii) Kuchunguza ruwaza ya upatanisho wa mofimu za kiima katika kishazi kikuu kwa kulinganisha na kishazi nomino.

iv) Kubainisha kama kanuni ya ukaguzi sifa katika nadharia ya uminimalisti inaelezea uamilifu wa kishazi nomino cha Kiswahili sanifu.

## 1.3 NADHARIA TETE

i) Vishazi nomino vya Kiswahili vyaweza kuainishwa katika kategoria zifuatazo:

a) Vishazi nomino rejeshi

b) Vishazi vya kwamba

c) Vishazi visoukomo

ii) Vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu vina majukumu sawa na ya virai nomino vya Kiswahili Sanifu katika sentensi.

iii) Kiima cha kishazi kikuu huathiri upatanisho wa kisarufi katika kishazi nomino.

iv) Kishazi nomino huathiriwa na yambwa ya kishazi kikuu kiupatanishi.

v) Nadharia ya uminimalisti ina mashiko katika uchanganuzi wa kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Katika sarufi ya Kiswahili Sanifu, vishazi tegemezi vimeainishwa na baadhi ya wataalamu kwa njia mbalimbali. Massamba na wenzake (1999) wameviainisha kwa misingi ya muundo na uamilifu wake. Kiuamilifu, anazungumzia vishazi elezi na vishazi rejeshi. Mohammed (2001) anaviainisha vishazi tegemezi kama vishazi bebwa na vishazi elezi. Polome (1967) anaporejelea vishazi nomino, anavieleza kama vishazi ambavyo vina upatanisho baina ya kiima na kiarifu inapowezekana. Polome (khj) anaelekea kudai kuwa kishazi nomino ni kishazi huru. Kutokana na kuwa kunaelekea kuwa na maelezo yasiyo wazi ya kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu, tumeona kuwa kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu kipashio hiki katika Kiswahili Sanifu.

Nadharia ya uminimalisti imetumika sana katika tafiti za Kiswahili zilizofanywa. Kwa kiwango kikubwa, nadharia hii imekubaliwa kama nadharia inayoweza kutumika katika uchanganuzi wa lugha ya Kiswahili. Ikumbukwe kwamba, Chomsky katika kuasisi nadharia hii amekuwa na nia ya kutafuta nadharia inayoeleza ubia katika lugha za

kilimwengu. Hata hivyo, tumetambua kwamba nadharia hii imetumiwa tu katika uchanganuzi wa sentensi sahili na hivyo inahitaji kujaribiwa zaidi katika uchanganuzi wa sentensi changamano.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA

Sentensi huundwa kwa vipashio mbalimbali kama vile mofimu, maneno, virai na vishazi. Kishazi ndicho kipashio kikubwa cha lugha katika uundaji wa sentensi. Katika Kiswahili Sanifu, vishazi ni vya aina mbili kuu navyo ni vishazi huru ama vishazi vikuu na vishazi tegemezi. Vishazi tegemezi vimegawanywa kiuamilifu na kupata kategoria mbalimbali: vishazi nomino, vishazi rejeshi (vishazi vumishi) na vishazi elezi (Leech na Svartik 2000:246). Utafiti huu umejikita katika uchunguzi wa vishazi nomino pekee ila pia tumevihusisha vishazi vikuu vinavyovibeba.

Nadharia tuliyotumia katika uchanganuzi huu ni nadharia ya uminimalisti ambayo iliasisiwa na Chomsky (1993, 1995). Katika kutumia nadharia hii tumezingatia kipengele muhimu cha ukaguaji sifa ambacho ndicho kimetuelekeza kuubainisha ufaafu wa nadharia hii katika uchanganuzi wa kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu. Pia, tumefaidika sana na uhusiano wa kimofosintaksia wa nadharia hii hasa katika uchunguzi wa upatanisho wa kisarufi wa kishazi nomino na kishazi kikuu.

Utafiti wetu umejikita katika Kiswahili Sanifu kwani, kama tulivyoeleza awali, lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi ambazo zinaweza kushugulikiwa ila hatutazishughulikia lahaja hizo.

## 1.6 MISINGI YA NADHARIA

Nadharia tuliyotumia katika utafiti huu ni nadharia ya uminimalisti ambayo iliasisiwa na Chomsky (1993, 1995). Tumeichagua nadharia hii kwa misingi ya kuwa inaelekea kuwa ndiyo nadharia inayofaa zaidi katika uchanganuzi wa lugha ambishibainshi kama Kiswahili. Ufaafu wake unatokana na sifa ya nadharia hii ya kushughulikia kipengele cha kimofolojia katika sintaksia.

Binadamu ana uwezo wa lugha ambao upo katika akili yake. Uwezo huu wa lugha una vitengo vya jumla viitwavyo umilisi na utendaji. Umilisi ni ujuzi alio nao msemaji wa lugha. Huu humpa uwezo wa kusawiri uhusiano wa vipashio vya kiisimu na kuvichanganua, kuviunda na kueleza au kufafanua muundo wa lugha yake katika sarufi. Msemaji anaweza kuunda idadi isiyo na kikomo ya sentensi akitumia idadi thabiti ya kaida. Umilisi humwezesha msemaji asili kufanya ukaguzi kuhusu usarufi wa usemi ambapo welewa wake humsaidia kuamua kama sentensi zimeundwa vema kisarufi au la. Utendaji, kwa upande wake, ni matumizi halisi ya lugha. Utendaji hujengeka zaidi katika muundo wa lugha kwa matumizi bora na huegemea zaidi katika dhana za kitamaduni na kikaida kuliko usanifu wa sentensi. Ni katika uelewa huu ambapo Chomsky anaegemeza mawazo yake ya nadharia ya uminimalisti.


Tangu miaka ya hamsini, Chomsky amejitahidi sana kuibuka na nadharia mbalimabli za sarufi bia. Mwaka wa 1957,Chomsky alibuni nadharia ya sarufi miundo na kuifanyia marekebisho katika miaka ya 1965 na kuibuka na Sarufi Zalishi Geuza Maumbo(SZGM). Nadharia hii ilifanyiwa marekebisho katika miaka ya sabini na kukaibuka na Nadharia ya

Wastani ambayo nayo ilifanyiwa marekebisho na kuibuka na Nadharia ya Wastani Panuzi. Nadharia hizi zote zilishughulikia Sarufi Miundo Virai. Matatizo yaliyosheheni katika nadharia hii yalifungulia mlango nadharia ya Umilikifu na Masharti (tangu sasa U&M) katika mwaka wa 1980. Nadharia hii ilikuwa na vitengo mbalimbali navyo ni X-baa, thita, uhusika, masharti, umilikifu, ufunge na utawala ( Horrocks 1987:101). Kufikia mwaka wa 1995, Chomsky aliibua nadharia ya uminimalisti ambayo, kwa hakika ni maendeleo wala si mkiuko wa dhima kuu ya sarufi zalishi. Dhima kuu ya sarufi zalishi tangu miaka ya 1960 imekuwa ni kuzua kanuni rahisi za lugha katika misingi ya sarufi bia. Hivyo, nadharia ya uminimalisti inaendeleza dhima hii ya urahisishaji.

Nadharia ya uminimalisti ina misingi yake katika mfumo wa Kanuni na Vigezo ambao ulitumika sana katika tafiti za kisintaksia katika miaka ya 1980. Uminimalisti kama nadharia ya kiisimu ni wazo la hivi karibuni la Chomsky (1995c). Nadharia hii ina misingi yake katika nadharia ya Kanuni na Vigezo, kama tulivyotangulia kutaja, na hasa kanuni ya iktisadi na kanuni ya ufafanuzi wa kina. Kanuni ya ufafanuzi wa kina inadai kuwa hakuna vipashio visivyohitajika katika muundo wa sentensi. Hivyo, vipashio vyote huwa na uamilifu fulani uwe wa kisemantiki, kisintaksia au kifonolojia na ni lazima vipashio hivi vichanganuliwe kwa njia moja ama nyingine. Kanuni ya iktisadi nayo ni hitaji la kijumla kuwa kila wakilisho na mifanyiko inayotumiwa kuvinyambua (vipashio) iwe ekevu iwekezekanavyo (Cook & Newson 1996:312).

Kwa mujibu wa kanuni ya iktisadi, wakilisho la kisintaksia la muundo lahitajika kuwa na vipashio vinavyohitajika tu. Ni kutokana na kanuni hii tunapoona muundo wa ndani na

muundo wa nje wa wakilisho ukitupiliwa mbali na kubakisha Umbo la kifonetiki (tangu sasa UF) na umbo la kimantiki (tangu sasa UM). Pia kunasalia leksikoni na mifanyiko ya kimkokotoo inayounda wakilisho la UF na UM kutokana na habari za leksikoni kwani kwa mujibu wa Chomsky (1995a:15), leksikoni na mifanyiko ya kimkokotoo hupatikana katika umilisi (Cook & Newson 1996:314). Hivyo tofauti na mchoro wa T katika U&M, mchoro wa uminimalisti waonekana kuwa hivi:





Katika mchoro huu, mistari hii inawakilisha mifanyiko inayojenga wakilisho la UF na UM kutokana na leksikoni.


### 1.6.1 Mifanyiko Ya Kimkokotoo

Kitengo cha leksikoni huhifadhi leksika na habari zote za kimofosintaksia kuhusu nomino na vitenzi. Kundi la vipashio vya kimofosintaksia na leksika huchaguliwa katika mfanyiko uitwao numerali. Katika mfanyiko huu, ni muhimu vipashio vyote vinavyochaguliwa vitumike iwapo sentensi sanifu itaundwa. Muungano hutokea na

kuunganisha vipashio mbalimbali. Muungano huu huunda miundo ya virai ambavyo navyo huungana ili kuunda muundo mmoja tu sanifu. Katika mtazamo huu wa uminimalisti, ikumbukwe kwamba kanuni zilizopatikana katika U&M za uvurumishaji na umbo la ndani zilitupiliwa mbali. Badala yake, uminimalisti unabakisha nadharia ya X-baa (Chomsky 1993:6). Sifa ya X-baa inayobakishwa ni ile ya uhusiano wa spesifya-kichwa na kichwa-kichwa. Leksika zilizochaguliwa kutoka leksikoni hubadilishwa na kuwa katika uhusiano wa spesifaya-kichwa au kichwa-kijalizo (Chomsky 1993) kama inavyobainika katika mchoro huu:




Mifanyiko ya uundaji ni tofauti na kanuni ya uvurumishaji kwani mifanyiko hii hutokea kutegemea haja. Miundo huundwa tu iwapo itaidhinishwa na habari za kimofosintaksia au leksika kutoka leksikoni. Hivyo mchoro usiokuwa na kijalizo na wenye kichwa unawezekana iwapo hakuna haja ya kupima uhusika. Kwa mfano:




Nadharia hii haikubali nafasi tupu kwa sababu ya kanuni ya iktisadi. Vipashio visivyokuwapo havipewi nafasi ya kichwa.

Katika mfanyiko huu wa kujenga miundo, usogezi ni hatua ya muhimu. Tofauti na ilivyo katika U&M, maneno husogezwa kwa madhumuni ya ukaguzi. Haja ya ukaguzi huumba nafasi katika ujenzi wa miundo, kwa mfano nafasi ya spesifaya ni muhimu tu iwapo kuna vipashio vinavyohitaji ukaguzi wa uhusika. Usogezi hukagua usanifu wa sifa dhahania za uambishaji kama vile Upatanishi (UP) na Njeo (NJ) dhidi ya nafasi zilizopewa kisintaksia katika muundo wa sentensi. Hivyo, sifa hizi husogezwa kwa UPk, NJ na UPy ili kuondoa sifa dhahania katika UF. Usogezi unaweza kutokea katika hatua yoyote ya uundaji hadi UF na UM.

Usogezi huongozwa na kanuni ya iktisadi ambayo hujumlisha kanuni zingine ambazo ni: kanuni ya usogezi mfupi, kanuni ya kuchelewesha, kanuni ya ubinafsi na kanuni ya kimbilio la mwisho. Kanuni ya usogezi mfupi inasema kuwa usogezi unatokea tu hadi mahali karibu zaidi panapostahili. Kanuni hii hukubalia usogezi hadi nafasi husika: inasema, sharti ifanye usogezi "mfupi kabisa" (Chomsky 1995b:401). Kanuni ya kuchelewesha huhakikisha kwamba usogezi hutokea tu pale ambapo pana haja yake na kama umeidhinishwa na ushahidi wowote wa kimofosintaksia ama leksika kutoka kwa lugha husika. Kanuni ya kimbilio la mwisho huhakikisha kuwa usogezi mfupi unapendelewa kuliko ule mrefu. Kanuni ya ubinafsi nayo uhakikiksha kuwa usogezi unawezekana tu kama mahitaji ya usogezi wa vipashio yametimizwa katika mdhihiriko wazi na mjumuiko (Chomsky 1995:200).


Baada ya kujenga miundo, mifanyiko ya kimkokotoo hudhihirisha wazi habari za leksikoni katika mfanyiko uitwao mdhihirisho wazi. Mdhihirisho huu hutokea katika mijumuiko miwili ambayo ni UF na UM. Mdhihirisho wazi ni mfanyiko ambao huchukua muundo ambao haujakamilika na wenye habari za kifonetiki na kisemantiki kutoka kwa leksikoni na kuugawanya hivi kwamba kuna wakilisho lenye habari za kifonetiki na lingine lenye habari zilizosalia. Habari za kisemantiki hazikubaliki katika UF wala za kifonetiki hazikubaliwi katika UM. Iwapo matakwa haya yatatimizwa, basi unyambuzi ule hujumuika katika kiwango cha mjumuiko la sivyo, umbo lile hugongana. Mchoro ulio hapa chini unaonyesha jinsi mifanyiko hii ya kimkokotoo hufuatana.




### 1.6.2 Mofolojia Na Uminimalisti

Kama tulivyotangulia kusema, nadharia ya uminimalisti ina sifa ya kimofosintaksia ambayo huchukulia kwamba sifa za uambishi hupewa vitenzi na nomino katika leksikoni. Pia, inachukulia kuwa vitenzi na nomino zilizoambishwa tayari huzalishwa katika KT chini ya vichwa vyao. Vipashio vya NJ na UP vimejumuishwa katika kitenzi katika leksikoni na huitwa sifa za kitenzi (*V-features*). Uamilifu wa sifa hizi ni kukagua sifa za kitenzi baada ya kuchaguliwa katika leksikoni na kabla ya kutoka katika UF na UM. Kuhusiana na UP, nadharia hii hudai kuwa lugha zina sifa thabiti au sifa dhaifu. Sifa

thabiti hudhihirika katika UF ilhali sifa dhaifu hazidhihiriki. Hivi ni kusema kwamba lugha zenye sifa thabiti, kama Kiswahili, hulazimisha usogezi wa kitenzi ili kutupilia mbali kitita cha sifa dhahania kabla ya mdhihirisho wazi katika UF ilhali lugha zenye sifa dhaifu hazihitaji kusogeza kitenzi kwani hakuna sifa za kukaguliwa. Hivyo, kitenzi hudhihirika moja kwa moja katika UF na UM. Chomsky (1993:7) alipendekeza muundo msingi mpya wa sentensi kutokana na maelezo haya:




Kitita cha sifa dhahania ni kama ngeli, idadi (wingi au umoja) na nafsi zinazotofautisha na kutambulisha ukubaliano wa uamilifu wa majukumu ya kiima na yambwa. Nadharia hii inachukulia umuhimu wa lugha zenye uhusika unaoambishwa.

### 1.6.3 Kanuni Ya Ukaguzi Sifa

Katika nadharia ya uminimalisti, kama tulivyotangulia kutaja, mofolojia ambishi hupatakana katika leksikoni. Hivi ni kumaanisha kuwa maneno yanayochaguliwa kutoka

kwa leksikoni huwa yameambishwa tayari kinyume na ilivyokuwa katika nadharia awali za isimu. Katika nadharia ya U&M, vitenzi na nomino vinavurumishwa katika umbo la ndani ili vichukue sifa zake na kuonekana vyenye maana kisarufi katika umbo la nje (Schroeder 2002:16). Hivyo kanuni ya kukagua sifa hutumiwa tu katika kukagua sifa za maneno ambayo tayari yameundwa katika leksikoni ili kubainisha kama yanatimiza matakwa yaliyowekwa na lugha husika. Katika kanuni ya ukaguzi sifa vifundo amilifu humiliki kitita cha sifa dhahania (badala ya mofimu halisi).

Katika nadharia hii ya kukagua sifa, sifa za kisarufi hujumuisha sifa za kifonetiki, kisemantiki na kisarufi za maneno ambazo lazima zikaguliwe iwapo unyambuzi utakuwa na usarufi. Wasilisho la UF huwa na sifa zinazoweza kufafanuliwa kifonetiki nalo wasilisho la UM huwa na sifa zinazoweza kufafanuliwa kisemantiki. Haya ni matakwa yanayowekwa na kanuni ya sarufi bia iitwayo kanuni ya ufafanuzi wa kina. Kanuni hii hufafanua kuwa wasilisho la sentensi lazima liwe na elementi zote na zile tu zinazochangia moja kwa moja katika ufafanuzi wake katika kiwango kifaacho. Baadhi ya sifa za kisarufi za maneno zaweza kufafanuliwa katika kiwango cha UM (na hivyo kuchangia maana) na nyingine haziwezi kufafanuliwa katika unyambuzi wa wasilisho la UM ili kuhakikisha kuwa ule unyambuzi unakutana katika UM.

Nadharia hii huchukulia kwamba kategoria za maneno huwa na sifa tatu za kisarufi, nazo ni:

i) Sifa za kichwa au neno kuu ambazo hufafanua sifa zote za kisarufi za neno hilo.

ii) Sifa za kijalizo ambazo hufafanua vijalizo vinavyoweza kuchukuliwa na neno kuu.


iii) Sifa za spesifaya ambazo hufafanua spesifaya inayoweza kuchukuliwa na neno kuu. Chukulizi hii husuluhisha tatizo la jinsi ya kutupilia mbali sifa zisizoweza kufafanuliwa katika wasilisho la UM pamoja na mipaka ya kisarufi inayowekewa vichwa katika uchaguzi wao wa spesifaya na vijalizo. Kwa mujibu wa Chomsky (1995), sifa zote zisizoweza kufafanuliwa hubidi kukaguliwa katika umbo lifaalo la ukaguzi na kufutiliwa mbali. Bobaljik (1995) kama alivyonukuliwa na Kaviti (2004) anasema kichwa hukagua sifa za spesifaya na kijalizo chake. Sifa za spesifaya na kijalizo huchukuliwa kuwa haziwezi kufafanuliwa.

Nadharia hii inadai kuwa sarufi bia huweza kueleza bayana ni sifa gani za kichwa zinazoweza kufafanuliwa na zisizoweza kufafanuliwa. Kwa mfano sifa za idadi huweza kufafanuliwa ilhali sifa za uhusika haziwezi. Sifa za spesifaya za kichwa hukaguliwa dhidi ya sifa za kichwa cha spesifaya yake. Sifa za kijalizo hukaguliwa kwa sifa za kichwa cha kijalizo chake. Iwapo sifa zote zinafafanuliwa, basi unyambuzi hutosheleza matakwa ya kanuni ya ufafanuzi wa kina na hukutana katika UM. Iwapo kuna sifa zisizofafanulika, unyambuzi hugongana katika UM. Ukaguzi wa sifa na usogezi huruhusiwa kimofolojia au kileksika. Sifa iliyokaguliwa ndiyo hupita mkondo wa mifanyiko ya kimkokotoo lakini haitakiwi kuonekana katika UM kama vile sifa za jinsia, idadi, kundi n.k. Sifa za uhusika haziruhusiwi kuingia mifanyiko ya kimkokotoo baada ya kukaguliwa (Chomsky 1995:178). Ufuatao ni mfano wa ukaguzi wa sifa katika lugha ya Kiswahili:

3. Maria anataka chakula.

**Maria**- kiima **a**- ni kip. Nafsi 3 umoja **na**- kip. Njeo wkt. Uliopo **tak**- mzizi **a**- kiishio

**chakula** - yambwa



## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Kuna kazi nyinigi ambazo zimetusaidia katika kutayarisha tasnifu hii. Baadhi ya kazi hizo zimeshughulikia uchanganuzi wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kibantu, aidha kisintaksia ama kisarufi. Pia kuna kazi za kisarufi ambazo zimetupa mwanga mkubwa katika kuelewa vema vishazi kwa jumla na vishazi nomino hasa. Kazi hizi zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na zinajikita katika sarufi ya Kiingereza. Pia tumefaidika sana kutokana kazi ambazo zimeshughulikia nadharia ya uminimalisti.

Kazi ambazo zinashughulikia utafiti wa lugha ya Kiswahili na tulizopata manufaa kutoka kwake ni:

Tasnifu ya M.A. ya Mgullu (1990) ambamo ameainisha sentensi za Kiswahili na kuelezea sifa za kila mojawapo ya aina hizi. Anazifafanua sentensi hizi kwa kutumia nadharia ya sarufi geuza maumbo. Tumefaidika sana kutokana na ufafanuzi wake wa aina za sentensi za Kiswahili na hasa sentensi changamano na sifa zake. Mifano anayotumia katika kazi yake inatupa mwanga zaidi katika kazi yetu.

Jerono (2005) katika tasnifu yake ya M.A. alishugulikia kishazi arifu cha Kiswahili kwa kutumia nadharia ya X-baa ambayo ni mojawapo ya nadharia za U&M. Kazi yake pamoja na kutuangazia matumizi ya nadharia hii katika uchanganuzi wa kishazi huru cha Kiswahili, inatupa mwanga kuhusu muundo wa kishazi huru cha Kiswahili ambacho ni muhimu katika kazi yetu kwani ndipo kishazi nomino kinapoegemezwa.

Tasnifu ya Olali (1998) ya M.A. inashughulikia kirai nomino cha Kiswahili kwa mtazamo wa X-baa. Kazi hii inatupa mwanga mkuu katika kubainisha muundo wa kirai nomino cha Kiswahili. Ufahamu huu ni muhimu kwetu hasa katika kubainisha tofauti iliyopo baina ya kishazi nomino na kirai nomino cha Kiswahili.

Oichoe (2005) katika tasnifu yake ya M..A. anachunguza kimofosintaksia kirai tenzi cha Kiswahili kwa kukilinganisha na kirai tenzi cha Ekegusii. Kazi hii ina manufaa sana kwetu kwani inatuangazia zaidi muundo wa kirai tenzi cha Kiswahili. Isitoshe ametumia nadharia ya uminimalisti jambo ambalo linatufaidi sana katika kutathmini jinsi tunavyoweza kuitumia nadharia hii katika utafiti wetu.

Swaleh (2005) katika tasnifu yake ya M.A. amechunguza kishazi cha Kitikuu, ambayo ni mojawapo ya lahaja za Kiswahili kwa kutumia nadharia ya uminimalisti. Kazi hii imetusaidia katika uelewa wetu wa uchunguzi wa kishazi kwa mtazamo wa nahdaria ya uminimalisti.

Mutua (2005) katika tasnifu yake ya M.A. ameshughulikia kishazi tegemezi cha Kiswahili Sanifu kwa mtazamo wa X- baa. Kazi hii imetupa mwanga hasa katika uainishaji wa vishazi tegemezi na jinsi vinavyohusiana kimofosintaksia.

Mkude (2005) katika makala ya *Uchambuzi wa Sentensi za Kiswahili* anashughulikia masuala yanayohusiana na uchambuzi wa sentensi za Kiswahili. Anazungumzia vipashio

vya kisarufi vinavyounda sentensi za Kiswahili. Makala haya yametupa mwanga hasa katika masuala yanayoshughulikiwa katika uchambuzi wa sentensi.

Kazi ya Massamba na wenzake (1999) ni jaribio la kuchanganua sentensi za Kiswahili na vipashio vyake kwa kina. Kazi hii inashughulikia vipashio mbalimbali vinavyounda sentensi vikiwemo vishazi. Katika kazi hii, wataalamu hawa wanaviainisha vishazi vya Kiswahili na kutoa mifano kwa kila aina ya vishazi. Kazi hii imetufaidi sana katika kutupa mwelekeo wa uainishaji wa vishazi vya Kiswahili.

Mohammed (2001) ameshugulikia aina za sentensi za Kiswahili na uundaji katika kazi yake ya *Modern Swahili Grammar*. Isitoshe, ameshughulikia vishazi vya Kiswahili kwa kuonyesha muundo wake. Pia, ameviainisha vishazi vikuu vya Kiswahili na vishazi na vishazi tegemezi vya Kiswahili na akapiga hatua zaidi na kuviainisha vishazi tegemezi.

Vitale (1981 ) ameshughulikia sentensi za Kiswahili. Katika kazi yake ya *Swahili Syntax* pia, ameshughulikia kishazi tegemezi cha kwamba kwa kina. Kazi yake imetufaidi sana katika uelewa wetu wa kishazi hiki.

Polome (1967) ameshughulikia masuala mengi ya kisintaksia ya lugha ya Kiswahili. Katika kazi yake, tumefaidi sana maelezo aliyotoa ya kishazi na zaidi mifano ya Kiswahili anayotumia.

Kazi zilizotufaa zaidi katika kitengo cha kazi za kisarufi tulizopitia ni kama:

Quirk na wenzake (1972) katika kitabu chao *A Grammar of Contemporary English* wameshughulikia sentensi changamano, kwa mapana na marefu, katika sura ya kumi na moja. Wanasarufi hawa wameshughulikia aina mbalimbali za vishazi tegemezi vikiwemo vishazi nomino. Kazi hii imetupa msingi ya kuainisha vishazi nomino vya Kiswahili na kuubainisha uamilifu wake katika sentensi za Kiswahili.

Katika kazi nyingine, Quirk na Greenbaum (1973) wameainisha vishazi huru na vishazi tegemezi na kuvifafanua. Zaidi ya hayo, wametoa ufafanuzi wa kina wa vishazi nomino na kutoa mifano mwafaka katika lugha ya Kiingereza. Kazi hii imetunufaisha sana hasa katika kuufahamu uamilifu wa vishazi nomino katika sentensi.

DeCarrico (2000) katika makala ya *The Structure of English: Studies in Form and Function for Language Teaching* ameshughulikia masuala mengi ya kisarufi yakiwemo ya utegemezi katika sentensi changamano. Kazi hii imetusaidia katika kuumudu muundo wa vishazi nomino na uamilifu wake katika sentensi changamano. Mifano anayotumia ya Kiingereza imetufaidi katika uelewa wetu wa dhana hizi.

Huddleston (1984) katika kitabu chake *Introduction to English Grammar* ameyashughulikia masuala ya sarufi ya Kiingereza. Katika kazi hii, mwanasarufi huyu ameshughulikia vishazi huru na vishazi tegemezi kwa kina. Kazi yake imetufaidi sana katika kuelewa muundo wa vishazi tegemezi na vishazi huru kwa ujumla wake. Isitoshe, tumenufaika sana katika kutalii uamilifu wa vishazi mbalimbali katika sentensi.

Leech na Svartik (2000) katika *A Communicative Grammar of English* toleo la pili, wameshughulikia kwa njia ya moja kwa moja masuala ya muhimu yanayohusiana na vishazi kama vile uambatani na utegemezi. Mifano wanayotumia inatupa mwelekeo bora zaidi ingawaje ni ya Kiingereza, katika kufahamu vishazi nomino na vishazi vinginevyo.

Biber na wenzake (1999) pia ni kitabu kilichotufaidi sana na kutuongoza katika utafiti huu. Tumenufaika hasa na jinsi waandishi hawa walivyovishughulikia vipashio vya kisintaksia kwa kina na pia uanishaji wao wa vishazi tegemezi na hasa vishazi nomino. Zaidi ni jinsi walivyovihusisha vishazi nomino na vishazi vikuu vinavyovibeba.

Kazi zilizoshughulikia nadharia ya uminimalisti pia, zilitupa mwanga mkuu katika kuelewa misingi ya nadharia ya uminimalisti na jinsi ya kuitumia katika uchunguzi wetu. Baadhi ya kazi hizi ni zile zilizoandikwa na Chomsky mwenyewe kama vile Chomsky (1995) inayoifafanua nadharia hii kwa kina. Kazi hii inaeleza jinsi nadharia ya uminimalisti ilivyojitokeza kusuluhisha matatizo ya U&M. Ameeleza kwa undani matumizi ya kanuni ya iktisadi na vijikanuni vyake kwa mawanda makubwa yanayotusaidia kuifahamu nadharia ya uminimalisti zaidi.

Haegmann (1994) ameshughulikia kwa upana nadharia ya U&M pamoja na vijinadharia vyake. Baadaye, ameishughulikia nadharia ya uminimalisti kwa kuionyesha misingi yake. Kazi yake ilitufaidi katika jitahada zetu za kuielewa misingi ya nadharia ya uminimalisti.

Cook & Newson (1996) katika kazi yao *Chomsky's Universal Grammar,* wameelezea kwa njia ya kueleweka kwa urahisi nadharia ya uminimalisti na kuonyesha uhusiano wa nadharia hii na nadharia awali za Chomsky. Kazi hii pia, ilitupa msingi mwafaka wa kuielewa nadharia ya uminimalisti kwa urahisi zaidi.

Radford (1997a na 1997b) ni kazi ambazo zimeelezea kwa uwazi na kuirahisisha zaidi nadharia ya uminimalisti. Kazi hizi zilitufaa sana katika kuelewa hatua mbalimbali za mkokotoo na kanuni mbalimbali zinazotumika sana katika nadharia hii.

Tasnifu ya PhD ya Kaviti (2004) ambayo inatumia nadharia ya uminimalisti kuchanganua lugha ya Kikamba, inatupa mwanga zaidi katika kuielewa nadharia ya ukaguzi sifa katika nadharia ya uminimalisti na jinsi ya kuitumia katika uchanganuzi wa lugha.

Schroeder (2002) katika tasnifu yake ya PhD ametalii lugha ya Toposa katika mpangilio wa maneno katika sentensi akitumia nadharia ya kupima sifa za viambajengo vya uminimalisti. Kazi hii imetusaidia katika kuelewa uhusiano wa mofolojia na sintaksia na matumizi yake katika uminimalisti.

## 1.8 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu tumeufanya kwa kudurusu vitabu, majarida na majuzuu mbalimbali maktabani kwa mujibu wa kukusanya data. Tumepitia vitabu vinavyohusu nadharia tunayotumia ili tuweze kuielewa zaidi na jinsi ya kuitumia katika utafiti huu.

Pia tumesoma kazi mbalimbali za utafiti ili kuhakikisha kuwa tumepata kuchuja mawazo ya wasomi wengine ili kuyalinganisha na kuyalinganua na mawazo yetu.

## 1.9 UMUHIMU WA UTAFITI

Ni matumaini yetu kuwa utafiti huu umetoa mchango mkuu katika uchambuzi wa sentensi changamano za Kiswahili Sanifu. Huu ni uwanja ambao haujapata kutaliiwa sana kama ilivyo sentensi sahili za Kiswahili. Ni matumaini yetu kwamba utafiti huu umetoa changamoto kwa wasomi wengine kutafiti masuala mengi ambayo hayajashughulikiwa katika uwanja huu.

Utafiti huu pia, utasaidia sana wasomi wa sarufi ya Kiswahili pamoja na walimu wao katika kuuelewa muundo wa vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu na jinsi vinavyodhihirika katika sentensi za Kiswahili Sanifu.

# SURA YA PILI

# SENTENSI NA VIPASHIO VYAKE

## 2.0 UTANGULIZI

Kabla ya kuingilia ufafanuzi wa kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu, kama tulivyotaja katika sura ya kwanza, ni muhimu kufahamu vipashio vya kisintaksia vinavyohusiana na kishazi nomino. Katika sura hii tumefafanua dhana ya sentensi na kushughulikia vipashio vinavyounda sentensi. Ufafanuzi huu umetupa mwanga zaidi katika kuelewa muundo wa sentensi za Kiswahili na majukumu ya vipashio vinavyounda sentensi hizi. Pia, tumeshughulikia uainishaji wa ngeli za nomino kimofolojia na kisintaksia ili tuweze kuuelewa upatanisho wa kisarufi katika Kiswahili Sanifu vema.

## 2.1 DHANA YA SENTENSI

Kumekuwa na fafanuzi chungu nzima za dhana ya sentensi. Wanasarufi mapokeo waliifafanua sentensi kwa kusisitiza kuwa, sentensi huwasilisha wazo kamilifu. Katika kamusi ya *Routledge Dictionary of Language and Linguistics,* Bussmann (1996:427) anaeleza kwamba, wanamiundo wa Kimarekani wakimrejelea Bloomfield, walifafanua sentensi kama,

> "kipashio kikubwa kabisa cha kisintaksia kilicho huru ambacho hakiwezi kuegemezwa katika umbo lingine lolote la kisintaksia kwa kanuni yoyote ya kisarufi." (T.Y)

Wanamiundo hawa wanasema sentensi ni zao la uchanganuzi linalotokana na vipashio vidogo yaani fonimu, mofimu, maneno, virai hadi sentensi. Tunakubaliana na maelezo

kuwa sentensi ni kipashio huru na kwamba hakiwezi kuegemezwa katika umbo lingine. Hata hivyo suala la ukubwa na udogo wa vipashio ni suala ambalo ni tata na hatutaliingilia kwani halipo katika mipaka ya utafiti huu.

Wales (1989) anatupa mtazamo mwingine wa ufafanuzi wa sentensi anaposema kwamba sentensi ni kipashio chenye kiima na kiarifa na kuwa ni tofauti na kishazi kwani husimama pekee kama kipashio huru. Mawazo haya yanaafikiana na mtazamo tunaochukua katika kufafanua sentensi na pia kishazi. Hata hivyo hayaonyeshi tofauti iliyopo baina ya kishazi na sentensi.

Kwa jumla, ni wazi kuwa, kama asemavyo Crystal (2003:414), kadri fafanuzi zote zinazotolewa kuhusu sentensi zinaelekea kuathiriwa na mawazo ya Leonard Bloomfield, aliyeashiria uhuru wa sentensi kwa kusema kuwa, "haiwezi kwa mujibu wa muundo wowote wa kisarufi, kujumuishwa katika umbo kubwa zaidi la kiisimu". Mawazo haya yalidokezwa pia, na Huddleston (1989) aliposema kuwa sentensi haiwezi kupatikana ndani ya sentensi nyingine kwani ndilo umbo kuu zaidi la kisintaksia. Ukuu huu wa sentensi hauhusiani tu na ukubwa au udogo wa sentensi bali hasa uwezo wa sentensi yenyewe kujitosheleza kimawasiliano. Hivyo si urefu wa sentensi ulio muhimu, kwani inawezekana sentensi fupi, yaani yenye maneno machache, kujitosheleza kinyume na nyingine yenye maneno mengi zaidi. Kwa mfano:

1. Kisu kimepotea.
2. Kisu ambacho kilinunuliwa jana.

Sentensi 1 ina maneno mawili tu lakini inajitosheleza kimawasiliano kwani inawasilisha ujumbe ulio kamilika. Sentensi 2, licha ya kuwa na maneno mengi (manne), inahitaji kuegemezwa kwa utungo mwingine ili iweze kukamilika kimawasiliano kama vile,

3. Kisu ambacho kilinunuliwa jana kimepotea.

Katika utafiti huu, tutafafanua sentensi kama,

> "kipengele cha kisintaksia chenye kiima na kiarifa ambacho hakiwezi kuegemezwa katika muundo mwingine wa kisintaksia kwa kutumia kanuni yoyote ya kisarufi na ambacho kinajitosheleza kimawasiliano."

Kwa mfano:

4. Amina ni mtoto wa tajiri.
5. Amina ataolewa na Ali, ambaye ni mtoto wa maskini.
6. Ingawa Amina ni mtoto wa tajiri, ataolewa na Ali, ambaye ni mtoto wa maskini.

Mifano hii ni ya sentensi kwani kama tunavyoona, inajitosheleza kimawasiliano. Hata hivyo ibainike kuwa ingawa 4 na 5 ni sentensi, katika 6 si sentensi tena kwani zinatumiwa kuunda kipashio kikubwa zaidi. Hivyo hadhi yake inashushwa na kuwa kishazi ili kuunda sentensi. Sentensi katika sintaksia ndicho kipashio chenye hadhi ya juu zaidi.

## 2.2 VIPASHIO VYA SENTENSI

Kama tulivyodokezea mwanzoni mwa sura hii, sentensi huundwa kwa vipashio mbalimbali. Vipashio hivi ni vishazi, virai, maneno na hata mofimu. Katika sehemu hii

tutavifafanua vipashio hivi huku tukizingatia dhima yake katika uundaji wa sentensi za Kiswahili Sanifu.

### 2.2.1 MANENO

Dhana ya neno inaweza kuelezwa kwa misingi mbalimbali kama waelezavyo Habwe na Karanja (2004) kwani utata wa kueleza maana ya dhana hii hutokea katika kutofautisha baina ya neno na vipashio vingine vya kiisimu. Hata hivyo, ni wazi kuwa neno ni kipashio cha kiisimu kinachoundwa na mofimu moja au zaidi. Hatutajikita katika ufafanuzi wa dhana ya neno. Kuna aina nyingi za maneno na kila lugha huwa na idadi tofauti ya maneno. Katika lugha ya Kiswahili, wanazuo mbalimbali wameainisha maneno katika makundi mbalimbali kulingana na maana na utendakazi wake. Baadhi yao wamedai kwamba kuna makundi saba ya maneno (Nkwera 1978, Kapinga 1983, Massamba na wenzake 1999) huku wengine wakiainisha makundi nane. Hawa ni kama Mgullu (1999), Mohammed (2001) na Habwe na Karanja (2004) miongoni mwa wengine. Katika utafiti huu tutaainisha maneno katika makundi nane yafuatayo:

I. Nomino
II. Vivumishi
III. Viwakilishi
IV. Vitenzi
V. Vielezi
VI. Viunganishi
VII. Vihusishi
VIII. Vihisishi

## I. NOMINO

Nomino ni maneno ambayo hutaja vitu, watu, mahali, vyeo, dhana na hata vitendo. Nomino huwapa watu na vitu utambulisho. Katika sentensi, nomino hutumika kama kiima, kijalizo ama yambwa tendwa au tendewa. Nomino ni muhimu sana katika mawasiliano kwani ndiyo hutambulisha kinachozungumziwa. Katika Kiswahili Sanifu nomino huweza kudhihirika wazi ama zikaashiriwa kwa kiambishi mwafaka ambacho hupatikana katika kitenzi. Nomino za Kiswahili zimeainishwa katika makundi mbalimbali yanayojulikana kama ngeli. Ngeli za Kiswahili kama za lugha nyingine za Kibantu, huweza kuainishwa kwa misingi ya kisemantiki, kisintaksia na kimofolojia. Kisemantiki, mkazo hutiliwa katika maana ya nomino. Hatutajishughulisha sana na uainishaji wa kisemantiki wa ngeli katika utafiti huu. Badala yake tutazingaatia uainishaji wa ngeli za Kiswahili kimofolojia na kisintaksia kwani utafiti huu utajishughulisha na mofosintaksia ya kishazi nomino.

### Uainishaji Wa Ngeli

Uainishaji wa ngeli kimofolojia huzingatia hasa kiambishi awali cha nomino katika umoja wake na wingi wake. Kimofolojia, nomino ambayo huwa na viambishi ngeli vinavyofanana huwekwa katika ngeli moja. Makundi haya ya ngeli hupewa nambari. Kisintaksia, nomino za Kiswahili huainishwa kwa kuzingatia viambishi vya upatanisho wa kisarufi katika tungo. Hivyo, nomino ambazo kimofolojia zingekuwa katika kundi tofauti hujipata katika kundi lingine kisintaksia. Kwa mfano:

7. a) Mtoto huyu anapenda kusoma.

b) Kipofu huyu anatembea peke yake.

Kimofolojia, nomino *mtoto* na *kipofu* huwekwa katika makundi tofauti lakini kisintaksia nomino hazi zipo katika kundi moja kwa sababu ya viambishi vya upatanishi wa kisarufi vinavyotumiwa.

Tutazifafanua ngeli hizi kwa kuzingatia kigezo cha kimofolojia na cha kisintaksia kwa pamoja. Ngeli za Kiswahili Sanifu zimeainishwa katika makundi kumi na nane, kwa kutumia kigezo cha kimofolojia.

**Ngeli ya 1 {mu}**

Ngeli hii huchukua nomino zenye kiambishi ngeli **{mu}.** Kwa mfano neno {mu + ungwana}. Hata hivyo, kiambishi ngeli huweza kuwa na alomofu zake ambazo hutokana na mabadiliko ya kimofofonolojia[1] kutegemea mzizi wa nomino husika. Baadhi ya alomofu hizi ni kama {m} na {mw} kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

{mu + toto} ⟶ {**m**toto}

{mu + tu} ⟶ {**m**tu}

{mu + alimu} ⟶ {**mw**alimu}

{mu + ana} ⟶ {**mw**ana}

Kisintaksia, nomino katika ngeli hii huchukua kiambishi cha upatanisho wa ngeli {a} au {yu}. Kwa mfano:

8. Mtoto hu<u>**yu**</u> mzuri <u>**a**</u>naimba sana.

---

[1] Mabadiliko ya kimofofonolojia hutokea panapokuwa athari baina ya vipengele vya kifonolojia na vya kimofolojia. Kwa mfano {mu + alimu} inakuwa {mwalimu}. Hatutayaingilia mabadiliko haya kwani yako nje ya upeo wetu.

9. Kijana **yu**le **a**lishinda zawadi.

**Ngeli ya 2 {wa}**

Ngeli hii huwakilisha wingi wa nomino za ngeli ya 1. Kiambishi cha ngeli hii ni {**wa**}. Kiambishi hiki pia huwa na alomofu **{w}**. Mifano ya nomino zinazopatikana katika ngeli hii ni kama vile:

{wa + toto} ⟶ {**wa**toto}

{wa + ana} ⟶ {**w**ana}

Katika sentensi, nomino katika ngeli hii hupatanishwa kwa kutumia kiambishi cha upatanisho wa ngeli **{wa}**. Mathalan:

10. Wanahabari **wa**le **wa**liokuwa Eldoret **wa**megoma.

11. Ng'ombe **w**ote **wa**lipelekwa malishoni.

**Ngeli ya 3 {mu}**

Katika ngeli hii, hupatikana nomino zenye kiambishi ngeli **{mu}**. Mofimu hii huwa na alomofu zake ambazo ni [mu}, [mw] na [m]. Mifano ya nomino katika ngeli hii ni:

{mu + undo} ⟶ {**mu**undo}

{mu + ti} ⟶ {**m**ti}

{mu + embe} ⟶ {**mw**embe}

Kisintaksia, nomino katika ngeli hii huchukua mofimu ya upatanisho **{u}**. Kwa mfano:

12. Mti **u**le mrefu **u**likatwa juzi.

13. Tuta**u**ng'oa mmea hu**u** **u**lioharibika.

**Ngeli ya 4 {mi}**

Nomino katika ngeli ya 3 huchukua wingi wake katika ngeli hii ya 4. Kiambishi ngeli cha ngeli hii ni **{mi}**. Mifano ya nomino za ngeli hii ni:

{mi + undo} ⟶ {**mi**undo}

{mi + ti} ⟶ {**mi**ti}

{mi + embe} ⟶ {**mi**embe}

Nomino katika ngeli hii hupatanishwa kwa kutumia mofimu **{i}** na alomofu yake **{y}**. Kwa mfano:

14. Miembe hiyo iliyokatwa ililileta hasara kubwa.

15. Miti yote imefurika.

**Ngeli ya 5 {ji}**

Kiambishi ngeli cha nomino za ngeli hii ni **{ji}** kama ilivyo katika {**ji**ko}, {**ji**no}n.k. Hata hivyo kuna baadhi ya nomino katika ngeli hii ambazo hazichukui kiambishi ngeli bali huchukua mofu kapa {ø}, kwa mfano:

{ø + goti} ⟶ {goti}

{ ø+ chungwa} ⟶ {chungwa}

16. Gari **li**libingiria **li**kaingia mtoni.

17. Jino **li**na**lo**uma sharti **li**ng'olewe.

**Ngeli ya 6 {ma}**

Nomino ya ngeli ya 5 hupata wingi wake katika ngeli ya 6 ambayo mofu yake ni {**ma**}. Mofu hii hujidhihirisha katika nomino zote za ngeli hii. Alomofu ya mofu hii ni {**m**}.

Kwa mfano:

{ji + cho} ⟶ {**ma**cho}

{ø + tawi} ⟶ {**ma**tawi}

{ji + ko} ⟶ {**m**eko}

Kisintaksia, nomino katika ngeli hii hupatanishwa kwa mofu **{ya}** na alomofu yake **{y}**.

Kwa mfano:

18. Magari **ya**li**yo**nunuliwa juzi **ya**meibiwa.

19. **Ya**peleke meko ha**ya** jikoni.

**Ngeli ya 7 {ki}**

Kiambishi ngeli cha nomino katika ngeli hii ni {**ki**} na alomofu yake {**ch** }. Mofimu hizi pia, ndizo hutumiwa katika upatanisho wa kisintaksia. Kwa mfano:

{ki + beriti} ⟶ {**ki**beriti}

{ki + ombo} ⟶ {**ch**ombo}

20. Kitanda ali**cho**nunua juzi **ki**mevunjika.

21. Chakula hi**ki** ni **ki**ngi sana.

**Ngeli ya 8 {vi}**

Kiambishi ngeli cha nomino katika ngeli hii ni {**vi**} na alomofu zake ni {**vy**}. Kwa mfano:

{vi + atu} ⟶ {**viatu**}

{vi + akula} ⟶ {**vyakula**}

Kiambishi cha upatanisho cha ngeli kisintaksia katika ngeli hii ni sawa na kiambishi cha kimofolojia, kama ilivyo katika ngeli ya 7. Kwa mfano:

22. Vyakula **vy**ote **vi**liharibika na **vi**kamwagwa.

23. Hamisi alipewa viberiti **vi**ngi **vi**li**vyo**tengenezewa Marekani.

**Ngeli ya 9 {n}**

Nomino katika ngeli hii yaweza kuchukua kiambishi ngeli **{n}** ama zikawa na mofu kapa **{ø}**. Kwa mfano:

{n + nguo} ⟶ {nguo}

{ø + kalamu} ⟶ {kalamu}

Kisintaksia, nomino hazi huchukua mofu ya upatanishi **{i}** na alomofu yake **{y}**. Kwa mfano:

24. Nguo **y**angu **i**liraruka.

25. Nyundo hi**y**o ndi**y**o **i**litumiwa kung'oa misumari.

**Ngeli ya 10 {n}**

Ngeli hii huwakilisha wingi wa nomino yanayopatikana katika ngeli ya 9. Mofu inayotumika hapa ni **{n}.** Kimofolojia, mara nyingi mofu hii haidhihiriki kwa uwazi bali mofu ya upatanisho wa kisarufi **{zi}** ndiyo hudhihirika katika upatanisho. Kwa mfano:

{ø + nguo} ⟶{nguo}

{ø + kalamu} ⟶{kalamu}

26. Nguo zote zilifuliwa lakini zimenyeshewa.

27. Wape watoto hao kalamu zile zilizokuwa zimepotea.

**Ngeli ya 11 {u}**

Nomino zinazopatikana katika ngeli hii huchukua kiambishi ngeli **{u}** ambacho pia, huweza kujidhihirisha kama alomofu **{w}** katika baadhi ya nomino, kimofolojia. Kwa mfano:

{u + kuta} ⟶ {**u**kuta}

{u + araka} ⟶ {**w**araka}

Mofu hii pia ndiyo hutumika katika upatanisho wa kisintaksia. Mathalan:

28. Ali**u**jenga tena ukuta **u**liobomoka.

29. Mtoto ame**u**chukua wembe **w**enye makali **u**liomkata jana.

Nomino katika ngeli hii hupata wingi wake katika ngeli ya 10.

**Ngeli 14 {u}**[2]

Nomino katika ngeli hii huchukua kiambishi ngeli **{u}** na alomofu yake **{w}** kimofolojia na pia kisintaksia. Kwa mfano:

{u + rembo} ⟶ {**u**rembo}

{u + osia} ⟶ {**w**osia}

30. Urembo **w**ake **u**memtajirisha.

31. Uzuri **w**a aina hii ha**u**patikani kila mara.

---

[2] Ngeli ya 12 na ya 13 hazipatikani katika lugha ya Kiswahili ingawaje hupatikana katika lugha nyingine za kibantu. Ngeli hizi hurejelea udogo wa nomino au udunishaji wake. Suala hili hushughulikiwa katika ngeli ya 7 na ya 8 katika lugha ya Kiswahili.

**Ngeli ya 15 {ku}**

Nomino katika ngeli hii huundwa kutokana na vitenzi na hivyo huitwa vitenzi-nomino. Vitenzi - nomino hivi huundwa kwa kuambishiwa kiambishi awali **ku-**. Kiambishi hiki ndicho huchukuliwa na nomino katika ngeli hii na pia hutumiwa katika upatanisho wa kisintaksia pamoja na alomofu yake **{kw}**. Kwa mfano:

{ku + soma} ⟶ {kusoma}

{ku + imba} ⟶ {kuimba}

32. Kucheza **ku**le **ku**lipendeza wengi.

33. Kucheka **kw**ingi **ku**navunja mbavu.

**Ngeli ya 16, 17 na 18 {pa, ku, mu}**

Ngeli hizi tatu huwekwa pamoja kwa sababu ni ngeli zinazowakilisha mahali. Ngeli ya 16 huonyesha mahali mahususi na huchukua mofu **{pa}.** Kwa mfano {ha + pa} inakuwa {ha**pa**}. Ngeli ya 17 inachukua mofu **{ku}** na hurejelea mahali kusikodhihirika au kwa ujumla. Kwa mfano {ku + le} itakuwa ni {**ku**le}. Kiambishi ngeli **{mu}** na alomofu yake **{m}** huonyesha undani wa mahali. Kwa mfano {hu + mu} itakuwa {hu**mu**} ilhali {mu + le} itakuwa {**m**le}. Mofu hizi pia, ndizo hutumika kisintaksia. Kwa mfano:

34. Mahali ali**ko**enda ha**ku**julikani.

35. Afadhali tukae ha**pa** tuli**po**pazoea.

36. Nyoka ameingia hu**mo** pangoni.

## II. VIWAKILISHI

Viwakilishi ni maneno ambayo hutumiwa badala ya nomino. Kwa kuwa maneno haya hutumiwa kuwakilisha nomino, yanapotumiwa nomino zinazowakilishwa hazitajwi. Kueleweka kwa sentensi inayotumia viwakilishi hutegemea sana muktadha. Kwa mfano,

37. **Yale** ni mazuri kuliko **haya.**

Katika sentensi hii, ni muhimu kufahamu habari awali zitakazotuwezesha kufahamu kiwakilishi **yale** na **haya** vinawakilisha nomino gani la sivyo kutatokea utata wa maana.

## III. VIVUMISHI

Kivumishi ni kipashio cha kisintaksia ambacho hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino. Neno kivumishi limetokana na neno la Kiswahili 'vumisha' ambalo lina maana ya kutoa habari. Katika Kiswahili Sanifu, vivumishi hutokea baada ya kutajwa nomino yaani nomino + kivumishi kwa mfano:

a) Mtoto **mdogo**

b) Mayai **mengi**

Kivumishi huweza kudhihirika kama maneno ama vishazi rejeshi kama tutakavyoona katika sura ya tatu. Mathalan:

38. Mashamba **yale makubwa** yatagawanyiwa wakimbizi.

39. Mashamba **yaliyonyakuliwa na wakoloni** yatagawanyiwa wakimbizi.

## IV. VITENZI

Kitenzi ni kipashio cha kisarufi ambacho huarifu/hueleza jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi. Kitenzi ni sehemu muhimu ya kiarifu ambayo katika Kiswahili Sanifu ni lazima iwepo ili kukamilisha sentensi. Kitenzi ndicho hubeba habari za kimsingi katika sentensi na katika mawasiliano. Vitenzi vya Kiswahili hubeba habari nyingi sana kinyume na maneno mengine yote ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu vitenzi hivi huweza kupanuliwa kwa kuambishwa ama kunyambuliwa. Mfano wa vitenzi katika Kiswahili Sanifu ni:

40. Wanafunzi **wanasomea** mtihani wao wa mwisho wa muhula.

41. Padre wa kanisa letu **amewaita** akina mama wote kwa mkutano.

Vitenzi vya Kiswahili Sanifu vinaweza kuainishwa katika aina mbili ambazo ni:

i) vitenzi halisi

ii) vitenzi vishirikishi

Vitenzi halisi huonyesha vitendo maalum vinavyotendeka, wakati vinapotendeka, hali, kauli, uyakinishi au ukanushaji, anayetenda na hata anayeathiriwa na kitendo hicho. Habari hizi zote huweza kuonyeshwa kwa kutumia viambishi vinavyowakilisha sifa hizi. Mfano wa kitenzi halisi ni kama vile;

*42.* **Hatawaendeshea**

43. Halima alikuwa **akiwashughulikia** wageni.

Vitenzi halisi pia huweza kugawika katika aina mbili: vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi. Vitenzi vikuu ni vitenzi vinavyobeba ujumbe wa kitendo kinachorejelewa pamoja na habari nyingine za muhimu kama yambwa, mtenda, njeo na labda hali. Kwa mfano:

44. Mama alikuwa **anawatengenezea** malazi wageni wake.

45. Magari yalikuwa **yakiendeshwa** kwa kasi sana.

Hata hivyo, kunavyo vitenzi vingine vikuu visivyobeba habari hizi na huchukua kiambishi **KU** mwanzoni mwa kitenzi tu. Kwa mfano,

46. Mariamu anapenda **kuongea** sana.

47. Utakuja **kujuta** baadaye.

Vitenzi visaidizi, kwa upande wake, husaidia kuleta maana kamili ya kitenzi kikuu. Kitenzi kisaidizi huonyesha uyakinishi na hali ya kitenzi kikuu. Katika sentensi, kitenzi kisaidizi hutangulia kitenzi kikuu na ni lazima viambatane sambasamba kwani kitenzi kisaidizi hakiwezi kujisimamia kimaana pekee. Kwa mfano:

48. Waziri **anapenda** kutangaza msimamo wake.

49. Mashaka **alikuwa** anampenda Hamisi sana.

Vitenzi visaidizi ni kategoria ya kiuamilifu kwani kwa hakika, hakuna vitenzi ambavyo hufanya kazi ya vitenzi visaidizi pekee katika Kiswahili Sanifu. Aidha huwa ni vitenzi vikuu kama katika (48) ama ni vitenzi vishirikishi kama katika (49).

Vitenzi vishirikishi huonyesha hali, tabia au mazingira. Pia huashiria vyeo au sifa za wahusika. Vitenzi vishirikishi vyaweza kujumuisha vitenzi vya kuwa, vitenzi vya kuwa na na vitenzi vya kuwa mahali. Mathalan:

50. Huyu **ni** mwalimu.

51. Malik **ana** vitabu vizuri sana.

52. Nadia **alikuwa** shambani.

Kama wasemavyo Habwe na Karanja (2004:174), vitenzi vishirikishi havina uarifishaji mkamilifu na kwa sababu hiyo hujalizwa na kijalizo. Kijalizo hiki huwa aidha ni nomino, kirai nomino au kishazi nomino.

Vitenzi vya Kiswahili pia vyaweza kuainishwa kwa mujibu wa uelekezi wake yaani vitenzi elekezi na vitenzi visoelekezi. Vitenzi elekezi ni vile vinavyohitaji kuchukua yambwa ili viweze kukamilika kimawasiliano. Kwa mfano:

53. Dereva **anaendesha** gari.

Katika mfano (53), kitenzi *anaendesha* hakiwezi kujitoshelesha kimawasiliano bila yambwa. Hivyo sentensi **Dereva anaendesha* itakuwa si kamilifu kimawasiliano ama iwe na maana nyingine tofauti kimawasiliano. Vitenzi visoelekezi ni vitenzi visivyohitaji yambwa kukamilika kimawasiliano. Mathalan:

54. Achieng' **anaimba** vizuri sana.

Katika kuainisha vitenzi vya Kiswahili Sanifu mtazamo mwingine unaoweza kutumiwa ni ule uanishaji wa kisemantiki wa vitenzi. Katika uainishaji huu, tunaweza kupata vitenzi vifuatavyo kwa mujibu wa Biber na wenzake (1996):

i) Vitenzi Tendi

Hivi ni vitenzi ambavyo huashiria vitendo na matukio ambayo, mara nyingi, yaweza kuhusishwa na hiari. Mathalan: lete, piga, nunua, hama, enda, kuja, n.k.

Vitenzi hivi vyaweza kuwa elekezi au visoelekezi. Kwa mfano:

55. Baba **amemnunulia** Mwangi nyumba kubwa.

Mara nyingi kiima cha vitenzi hivi huwa ni mtenda kama katika sentensi (55).

ii) Vitenzi Usemi

Vitenzi vya usemi vipo katika kategoria ya vitenzi vya hiari ambavyo huhusisha vitendo vya usemi kama vile kuandika na kuongea. Mathalan: uliza, sema, ita, eleza, taja, andika n.k.

iii) Vitenzi Sababishi

Hivi ni vitenzi ambavyo vinapotokea huleta hali mpya kama vile:

56. Mwalimu **amemruhusu** Judy kwenda chumbani.

iv) Vitenzi Vya Tukio

Vitenzi hivi hutaja matukio halisi ambayo hutokea bila hiari. Kwa hivyo, kiima chake mara nyingi huchukua nafasi ya mwathiriwa. Mathalan:

57. Maisha yake **yamekuwa** ya kubambanya.

v) Vitenzi Vya Uwepo

Hivi ni vitenzi ambavyo huarifu jinsi hali ilivyo baina ya vitu. Hivi hasa huwa ni vitenzi vishirikishi ambavyo hufuatwa na kijalizo na huwa na dhima ya kuhusisha kitu kimoja na kingine. Mathalan:

58. Umaskini **ni** hali ya kawaida mashambani.

vi) Vitenzi Vya Hali

Hivi ni vitenzi ambavyo huarifu hali ya kitendo au tukio na huripotiwa mara nyingi na kishazi jalizi. Mathalan:

59. Machozi **yalianza** kumbubujika.

vii) Vitenzi Dhahania

Vitenzi hivi hujumuisha vitendo vingi na matukio mengi anayoyapitia binadamu. Hata hivyo havihusishi vitendo halisi wala vya hiari. Vitenzi hivi hujumuisha vitenzi vya

utambuzi (mathalan: fikiri, jua), vitenzi vya hisia ambavyo huashiria matamanio na mitazamo mbalimbali kama vile penda, taka, tamani n.k. na vitenzi vya fahamu kama vile kuona, kusikia kuonja n.k.

### V. VIELEZI

Vielezi ni maneno yanayotoa maelezo zaidi kuhusu kitenzi, kivumishi ama kielezi kingine. Maneno haya hata hivyo, yana uhusiano wa karibu sana na vitenzi. Vielezi hueleza wakati tendo lilifanyika, jinsi lilivyofanyika, mahali lilipotokea na ni mara ngapi lilitokea. Kwa mfano;

60. Ng'ombe walipelekwa **malishoni alfajiri.**

61. Msichana yule mrembo **sana** ni rafiki yangu.

Ingawa sentensi inaweza kuwa kamilifu kimawasiliano bila vielezi, maneno haya hutumika sana katika sentensi kwa nia ya kuipanua sentensi hiyo na kuipa maana pana.

### VI. VIUNGANISHI

Viunganishi ni maneno ambayo hutumiwa kuunganisha aidha maneno mawili, virai ama vishazi. Viuganishi hugawika katika aina mbili; viunganishi viambatishi na viunganishi vitegemezi. Viunganishi hivi hutumiwa kuunda sentensi ambatano na sentensi tegemezi mtawalia[3]. Viunganishi viambatishi huunganisha maneno kwa maneno, virai au hata vishazi viwili huru au vya hadhi moja. Kiunganishi kiambatishi hutumiwa kuunda sentensi ambatano. Kwa mfano,

62. Baba **na** mama wanaenda Mombasa leo jioni.

63. Miti yote mirefu **na** yenye matawi mengi itakatwa.

[3] Uundaji wa sentensi ambatano na sentensi tegemezi utajadiliwa kwa kina katika sehemu 2.2.2.

64. Wanafunzi wamo darasani **lakini** mwalimu hajafika bado.

Katika sentensi 62, kiunganishi ambatishi *na* kimeunganisha maneno na katika sentensi 63 kikaunganisha virai vivumishi *yote mirefu* na *yenye matawi mengi*. Katika sentensi 64, vishazi viwili huru vimeunganishwa kwa kiunganishi ambatishi *lakini*.

Viunganishi vitegemezi kwa upande wake, ni viunganishi ambavyo huunganisha vishazi ambavyo vina hadhi tofauti. Hivi hutumiwa kuunda sentensi tegemezi. Kwa mfano,

65. Nandwa alisema **kwamba** hataolewa kamwe na mzee huyo.

Katika sentensi hii, neno *kwamba* ni kiunganishi tegemezi kwani kimetumiwa kuunganisha vishazi viwili vyenye hadhi tofauti.

## VII. VIHUSISHI

Vihusishi ni maneno ambayo huhusisha maneno au vifungu vya maneno. Aghalabu vihusishi, mara nyingi, hufanya kazi ya vielezi katika Kiswahili Sanifu. Vihusishi huhitaji kujalizwa. Vihusishi hivi, mara nyingi, hujalizwa na majina, viari nomino ama vishazi nomino. Mifano katika Kiswahili Sanifu ni:

66. Paka amelala **juu ya** kitanda.

67. Wanacheza **bila** wasiwasi.

## VIII. VIHISISHI

Istilahi hii inatokana na neno hisi lenye maana ya kupata msisimko fulani kutokana na aidha kuona, kusikia, kugusa, kuonja, kunusa na labda hata kuwaza. Maneno haya, basi, hueleza hisia mbalimbali apatazo binadamu katika shughuli zake za kila siku. Mifano ya maneno haya ni:

68. **Ala!** Kazi gani hiyo ya peni tatu?

69. **Masalaale!** Umewaona hao?

Maneno haya hayachukui viambishi vya upatanishi katika tungo na si ya lazima.

## 2.2.2 VIRAI

Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi lakini ambacho hakina muundo wa kiima-kiarifu. Kirai huundwa kutokana na mahusiano maalum ya maneno katika sentensi. Virai navyo vinapoungana pamoja huunda vishazi. Katika Kiswahili Sanifu, kuna aina tano za virai:

I. Kirai Nomino

II. Kirai Vumishi

III. Kirai Tenzi

IV. Kirai Elezi

V. Kirai Husishi

Tutavifafanua virai hivi kwa ufupi.

### I. KIRAI NOMINO

Kirai nomino ni kirai ambacho kimeundwa kwa nomino ama kiwakilishi kama kichwa. Nomino hiyo yaweza kuwa pekee ama ikawa imeandamana na mafungu mengine ya maneno.

Kirai nomino katika sentensi za Kiswahili Sanifu huwa na majukumu mbalimbali kisintaksia. Majukumu haya ni:

**i) Kiima**

70. **[Paka yule]** *n*i mgonjwa.

ii) **Yambwa tendwa**

71. Rubani aliona **[uwanja mbele yake]**.

iii) **Yambwa tendewa**

72. Alikubaliwa kumpikia **[Mariamu]** keki.

iv) **Kijalizo cha kiima**

73. Maira alikuwa **[mwalimu mzuri sana]**.

v) **Kijalizo cha kivumishi**

74. Mazishi [ya **[Bwana Katoli wa Katoni]**] yameahirishwa.

Katika sentensi 74, maneno yaliyokolezwa rangi ndiyo kirai nomino na yanajaliza kivumishi cha a-unganifu.

vi) **Kijalizo cha kihusishi**

Vihusishi kama tulivyoona katika sehemu ya 2.3.1 hujalizwa na nomino au virai nomino. Kwa mfano:

75. Yaweke maziwa yote [katika **chupa hizo mbili**].

vii) **Mrejeo sawa**[4]

Huu hutokea pale ambapo kirai nomino hutumiwa kurejelea kitu kilekile katika sentensi hata kama maana si sawa. Kwa mfano:

76. Tunasikitika kutangaza kifo cha aliyekuwa mkuu wa Shirika la Uvuvi, [**Bwana Mumias Kidongo**].

---

[4] Tumetafsiri 'apposition' kama mrejeosawa Taz. TUKI (1999:6)

## II. KIRAI TENZI

Kirai tenzi ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi au katika mahusiano ya kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno ( Massamba na wenzake 1999:101). Neno kuu katika kirai tenzi ni kitenzi. Dhana hii ya kirai tenzi hutumiwa pia, kuashiria kiarifa yaani kitenzi chenyewe na vipashio vingine vinavyokuja baada ya kitenzi chenyewe. Vipashio hivi vinaweza kuwa kirai nomino, kirai elezi, kirai husishi ama kishazi nomino.

Kisintaksia, kirai tenzi ndicho kipashio muhimu cha sentensi kwani ndicho hubeba ujumbe wa sentensi. Kirai tenzi cha Kiswahili Sanifu huweza kujisimamia pekee bila hata kirai nomino hasa kutokana na muundo wake wa kuweza kujumuisha baadhi ya sifa za kirai nomino. Mifano ya kirai tenzi ni:

77. [**Atawapakulia**].

78. Juma **[ameendesha gari lake kwa kasi]**.

## III. KIRAI VUMISHI

Kirai vumishi ni kirai ambacho kina kivumishi kama kichwa chake na kinaweza kuandamana na vivumishi vingine au visiwepo. Kirai vumishi chaweza kujitokeza kama neno moja (kivumishi) au zaidi ya moja yaani kivumishi na kielezi. Virai hivi mara nyingi hutokea ndani ya virai nomino. Hata hivyo, ni virai vinavyojisimamia. Kwa mfano:

79. Msichana **[yule mrefu mweupe]** alipatikana akiiba.

Virai vumishi huwa na majukumu yafuatayo kisintaksia:

**i) Kuvumisha nomino**

Kwa mfano:

80. Mwanafunzi **[mzuri mwenye bidii]** atafaulu mtihani *wake*.

**ii) Kijalizo**

Kwa mfano:

81. Daudi si **[mjinga sana]**.

## IV. VIRAI ELEZI

Kirai elezi ni kirai ambacho kichwa chake ni kielezi. Kielezi hiki chaweza kuandamana na vipashio vingine vya kukivumisha ambavyo vyaweza kuwa maneno, virai au hata vishazi. Vipashio hivi hasa hueleza kiwango. Kisintaksia, virai elezi huwa na jukumu la kutoa maelezo zaidi ya aidha kitenzi, kivumishi au hata kielezi. Kwa mfano:

82. Wageni walifika **[mapema sana]**.

## V. VIRAI HUSISHI

Kirai husishi ni kirai ambacho kimeundwa kwa kihusishi kama neno kuu na kijalizo ambacho mara nyingi ni kirai nomino. Virai husishi huweza kuegemezwa katika virai vingine vikubwa. Kwa mfano:

83. Kitabu kiko **[juu ya meza]**.

84. Alizungumza naye **[katika sherehe za kampuni *[pembezoni mwa nyumba]*]**.

Mara nyingi virai husishi hufanya kazi ya vielezi katika sentensi. Kwa sababu hii baadhi ya wataalamu huviainisha kama vielezi.

### 2.2.3. VISHAZI

Ufafanuzi wa dhana ya kishazi una mwingiliano mkubwa sana na wa dhana ya sentensi. Hii ni kwa sababu wataalamu mbalimbali huvipa vipashio hivi hadhi tofauti katika sintaksia. Kimuundo kishazi ni kipashio ambacho kina kiima na kiarifu. Hata hivyo, maelezo haya pia hutumiwa kueleza sentensi. Tutayatumia maelezo ya Crystal (2000:72) katika kubainisha tofauti kati ya sentensi na kishazi kihadhi anaposema kwamba kishazi ni dhana inayotumiwa kurejelea kipashio cha kisarufi ambacho ni kidogo kuliko sentensi lakini kikubwa kuliko kirai, maneno na mofimu. Kwa hivyo, kwa mujibu wa maelezo haya, sentensi ina hadhi ya juu kuliko kishazi. Huddleston (1984) anatupa maelezo zaidi kwa kusema kuwa mpaka baina ya sentensi na kishazi huingiliana iwapo kishazi kitajisimamia chenyewe (yaani sentensi sahili) bila kutumiwa kama kiambajengo cha sentensi na kupoteza hadhi hii kinapotumiwa katika sentensi nyingine. Wazo hili linajitokeza vema katika mfano tuliotoa awali (2.1: uk 26) ambao tumeurudia hapa:

85. Amina ni mtoto wa tajiri.

86. Ingawa Amina ni mtoto wa tajiri, ataolewa na Ali.

Tungo (85) ni kishazi chenye hadhi ya sentensi – yaani sentensi sahili kwa sababu kinasimama peke yake. Katika (86), *Amina ni mtoto wa tajiri* si sentensi sahili tena bali ni kishazi kwani kimetumiwa kama kiambajengo cha sentensi. Katika utafiti huu tutafafanua kishazi kama kipashio cha sentensi ambacho kina kiima na kiarifu na kinachoweza kuegemezwa kisarufi katika muundo mwingine wa kisintaksia.

Vishazi vimeainishwa kwa njia mbalimbali. Wanasarufi mapokeo waliainisha vishazi katika makundi mawili makuu:

i) Vishazi huru

ii) Vishazi tegemezi

Vishazi huru ni vishazi ambavyo hujitosheleza kimaana. Vishazi hivi huwa na maana kamili. Kimuundo, kishazi huru ni sawa na sentensi sahili. Kwa mfano:

87. Carol ni msichana mzuri.

Vishazi tegemezi ni vishazi ambavyo havijitoshelezi kimaana na hivyo huhitaji kuegemezwa katika kishazi kingine ili kukamilika kimaana. Vishazi tegemezi haviwezi kukaa peke yake kama sentensi maanake havieleweki. Kwa mfano:

88. Wanyama **[ambao wako hatarini]** watahamishwa kutoka mbuga hii.

89. Juma ameahidi **[kumweleza Martha yote]**.

Katika mifano tuliyotoa hapo juu, vishazi tegemezi vimewekwa katika mabano na haviwezi kujisimamia vikiwa peke yake.

Vishazi pia, huweza kuainishwa kimuundo kwa kuzingatia kitenzi kinachokijenga kishazi chenyewe. Katika uainishaji huu, kuna vishazi ukomo na vishazi visoukomo. Vishazi ukomo ni vishazi ambavyo kila mara huwa na kiima na kiarifa isipokuwa katika amri na udondoshajimaneno[5]. Vishazi huru karibu vyote, huwa ni vishazi ukomo. Kwa mfano:

90. Hamisi amekula samaki wawili.

Vishazi visoukomo havichukui kiima katika muundo wake. Vishazi hivi hudhihirishwa kwa kutumia kitenzi kisoukomo ambacho katika Kiswahili Sanifu hudhihirishwa kwa kiambishi **KU-**. Kitenzi kisoukomo hakichukui viambishi vya nafsi, njeo au hali. Kwa mfano:

91. Mama ameenda sokoni **[kununua mboga]**.

---

[5] Tumetafsiri udondoshaji maneno kama *ellipsis*

Vishazi pia, huweza kuainishwa kiuamilifu. Huu ni uainishaji ambao hutilia maanani majukumu ya kishazi katika sentensi. Kwa hakika uainishaji huu hulenga hasa vishazi tegemezi. Kwa mujibu wa uainishaji huu, tunapata aina tatu za vishazi katika Kiswahili Sanifu:

i) Vishazi Nomino

ii) Vishazi Rejeshi

iii) Vishazi Elezi

Vishazi nomino, ambavyo ndivyo hasa kiini cha utafiti huu, ni vishazi ambavyo huchukua nafasi ya nomino ama kirai nomino katika sentensi. Vishazi rejeshi hufanya kazi ya kuvumisha nomino katika sentensi. Hii ndiyo sababu wataalamu wengine huviita vishazi vumishi. Vishazi elezi navyo huchukua nafasi ya vielezi ama virai elezi katika sentensi. Hivi hujishughulisha hasa na kufafanua vitenzi, vivumishi na vielezi vingine katika sentensi. Ifuatayo ni mifano ya sentensi ambazo zina vishazi vilivyoainishwa kiuamilifu:

92. Jane alisema **[hataki kumwona Karisa]**. (kishazi nomino)

93. Mfalme **[ambaye ni Mwingereza]** amefika nchini. (kishazi rejeshi)

94. **[Usipokimbia]** hutampata. (kishazi elezi)

## 2.3 AINA ZA SENTENSI

Kimuundo, tutazigawa sentensi za Kiswahili Sanifu katika makundi matatu kama alivyozigawa Mgullu (1990). Makundi haya ni:

i) Sentensi Sahili

ii) Sentensi Ambatano

iii) Sentensi Changamano

Sentensi sahili, kwa mujibu wa Mgullu (1990), ni

> 'sentensi ambayo muundo wake wa ndani
> una kishazi kikuu bila vishazi ambishi ama ambatishi.'

Kwa mujibu wa Mohammed (2001:244), sentensi sahili ni sentensi yenye kishazi kimoja. Mkude (2005:239) anaelezea kuwa sentensi sahili ni sentensi yenye kiarifu kimoja. Anazidi kueleza kuwa ni sentensi yenye kitenzi kimoja. Kutokana na vijelezi hivi, ni wazi kuwa sifa kuu ya sentensi sahili za Kiswahili Sanifu ni kuwa na kiarifu ama kitenzi kimoja na kiima kimoja. Kwa mfano:

95. Maria anaenda shuleni.

Sentensi sahili za Kiswahili Sanifu mara nyingi huundwa kwa kitenzi kimoja tu katika utungo uitwao sentensi za neno moja. Katika sentensi za aina hii, kiima huashiriwa tu na kiambishi kirejeshi cha ngeli. Kwa mfano:

96. **A**tafika.

Katika sentensi hii, kiambishi kilichokolezwa rangi kinarejelea kiima cha sentensi hiyo. Hivyo, twaweza kusema kuwa, kiima katika sentensi sahili za Kiswahili Sanifu chaweza kuwa wazi ama kikawa kinaashiriwa tu yaani, si wazi. Uelewa huu wa sentensi sahili utatusaidia katika kuelewa muundo wa sentensi sahili za Kiswahili Sanifu na vishazi pia.

Kwa kuwa katika mawasiliano sentensi zinazotumiwa si sentensi sahili pekee, ni muhimu tufafanue muundo wa aina nyingine za sentensi. Iwapo vishazi viwili au zaidi

vitaunganishwa kwa kutumia viunganishi ambatishi, basi tutapata sentensi ambatano. Wazo hili linatolewa na Mgullu (1999) anaposema kwamba kama

> 'sentensi ambatano ni sentensi ambazo muundo wake wa ndani una vishazi viwili au zaidi huru vilivyo ambatanishwa kwa viambishi ambatanishi.'

Maelezo haya yanazua wazo muhimu la kuunganishwa kwa vishazi viwili huru. Tendo hili la kuunganisha vipashio vya hadhi sawa huitwa uambatani. Uambatani, kwa mujibu wa *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*, TUKI (1990), ni tendo la kuunganisha vipashio vya daraja moja.

Kwa mfano:

97. **[Tuliondoka mapema]** na **[tulifika kabla ya wengine]** lakini **[tulianza safari mwisho].**

Maneno yaliyotiwa katika mabano ni vishazi ambavyo vimetumiwa kuunda sentensi ambatano. Hivi ni vishazi vya daraja moja kwa sababu vyote ni vishazi huru. Katika sentensi ambatano, vishazi vya daraja moja ndivyo huunganishwa. Katika kueleza sifa za sentensi ambatano, Mgullu (1999) anasema kuwa sifa moja ya sentensi ambatano ni kuwa hakuna utegemezi katika vishazi vile.

Leech na Svartik (2000) wanasema kuwa uambatani waweza kuwa baina ya vipashio tofauti vya kisarufi kama vile vishazi, elementi za vishazi au maneno. Kwa mfano:

98. **a) Baba** na **mama** wanasafiri kesho.

    **b) Baba anaenda Mombasa** lakini **mama anaenda Kisumu**.

    c) Safiri **kwa basi** au **gari la moshi**.

Katika sentensi (98a), maneno yaliyokolezwa rangi ndiyo yaliyounganishwa ilhali katika sentensi (98b), vishazi vilivyounganishwa ni vile vilivyokolezwa rangi. Katika sentensi

(98c) elementi za kishazi ndizo zimeunganishwa. Uambatani huashiriwa na viunganishi ambatishi kama vile *au, na, tena, lakini* n.k

Aina ya tatu ya sentensi huundwa kwa utegemezi. Sentensi zinazoundwa kwa utegtemezi huitwa sentensi changamani. Kwa mujibu wa TUKI (1999), sentensi changamani ni

'sentensi yenye kishazi tegemezi kimoja au zaidi.'

Mohammed (2001) anafafanua sentensi changamani kama sentensi yenye kishazi kikuu na angalau kishazi kimoja tegemezi. Wazo kuu linalojitokeza katika vijelezi hivi ni dhana ya utegemezi.

Kwa mfano:

99. Musa anatia bidii masomoni **[ili aweze kufaulu maishani[**.

100. Mama **[aliyejifungua juzi]** amekamatwa na polisi.

Sehemu ya sentensi hizi iliyokolezwa rangi ni vishazi tegemezi vilivyoegemezwa kwa vishazi huru ili kupanua maana ya sentensi.

Utegemezi kwa mujibu wa Quirk na wenzake (1972:720) ni uhusiano usio sawa baina ya vishazi viwili, hivi kwamba kishazi kimoja ni sehemu ya kishazi kingine. Kishazi ambacho ni sehemu ya kingine huitwa kishazi tegemezi. Kama anavyoeleza DeCarrico (2000:143) hivi huitwa vishazi tegemezi kwa kuwa haviwezi kujisimamia kama sentensi huru bali ni lazima viegemezwe kwenye kishazi kikuu. Kutokana na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa utegemezi unahusiana na uunganishaji wa vishazi visivyo na uzito sawa. Utegemezi huashiriwa na viunganishi tegemezi kama vile *kwa sababu, ili, ingawa, -nge-, -ngali-*, n.k. Kwa mfano:

101. **Ingawa** John ni mtiifu, si mwaminifu.

Sentensi changamano pia, huweza kuundwa kutokana na utegemezi pamoja na uambatani wakati mmoja. Yaani kishazi chenye utegemezi chaweza kuunganishwa na kishazi huru ama na kingine chenye utegemezi kuunda sentensi changamani. Kwa mfano:

102. **[Ndege ambayo ilinunuliwa juzi kutoka Ujapani iliruka leo mara ya kwanza]** na [**haitaruka tena hadi miezi mitatu ipite**].

Katika sentensi (102) kishazi cha kwanza kina utegemezi ilhali kishazi cha pili ni kishazi huru. Huu ni mfano mmoja wa uchangamano.

## 2.4 HITIMISHO

Katika sura hii tumeshughulikia masuala muhimu ya sarufi kwa kuanganzia ufafanuzi wa dhana ya sentensi na vipashio vinavyoijenga sentensi. Isitoshe, tumeshughulikia uainishaji wa ngeli za Kiswahili Sanifu kimofolojia na kisintaksia. Ni matumaini yetu kwamba maelezo haya yametoa msingi mwafaka katika uelewa wa mada ambayo tumeshughulikia katika sura zinazofuata.

# SURA YA TATU

# KISHAZI NOMINO CHA KISWAHILI SANIFU

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura ya pili tuliainisha vishazi tegemezi kwa misingi ya uamilifu wake. Aina moja ya vishazi tegemezi tulivyoainisha ni vishazi nomino ambavyo tumeviainisha na kuvifafanua katika sura hii. Kisha tumetathmini majukumu ya vishazi nomino hivi kwa kuzingatia nafasi za agiumenti na nafasi zisizo za agiumenti zinazochukuliwa na vishazi nomino katika sentensi za Kiswahili Sanifu kwa misingi ya nadharia ya uminimalisti. Utathmini huu umetuelekeza katika kubainisha kama kweli vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu vina uamilifu sawa na wa virai nomino.

## 3.1 KISHAZI NOMINO

Kishazi nomino ni kishazi ambacho huelekea kuchukua nafasi sawa na ya kirai nomino katika sentensi. Kimuundo, kishazi nomino ni kishazi bebwa. Hivi ni kusema kwamba ni kishazi tegemezi ambacho ni kiambajengo cha kishazi kikuu[6]. Kishazi bebwa ni kishazi cha kimsingi katika uundaji wa sentensi. Iwapo kitaondolewa katika sentensi, sentensi hiyo itakosa maana. Kwa mfano;

1. Mama alisema **[kwamba atapitia dukani].**

Kishazi bebwa, *kwamba atapitia dukani,* kikiondolewa katika sentensi hii, kishazi kikuu *mama alisema* ndicho kitabaki na kitakuwa hakina maana kamili. Kwa hivyo tunaona kwamba kishazi bebwa ni cha msingi katika utunzi wa sentensi.

---

[6] Kwa maelezo zaidi juu ya kishazi bebwa rejelea Huddleston (1984:379 – 380)

Vishazi nomino katika Kiswahili Sanifu vyaweza kuainishwa katika kategoria tatu ambazo ni:

i) kishazi nomino rejeshi

ii) kishazi nomino kisoukomo

iii) kishazi nomino 'kwamba'

### 3.1.1. Kishazi Nomino Rejeshi

Kishazi nomino rejeshi kina msingi wake katika kishazi rejeshi. Kishazi rejeshi ni kishazi ambacho hupatikana katika KN na hurejelea nomino katika KN hicho. Katika Kiswahili Sanifu, kishazi rejeshi hubainishwa na kiwakilishi rejeshi amba- ama na kiambishi rejeshi -o-. Vishazi rejeshi vya Kiswahili Sanifu vyaweza kugawika katika kategoria tatu kama alivyoainisha Mgullu (1999):

a) vishazi rejeshi vyenye amba-

b) vishazi rejeshi vyenye kiambishi rejeshi awali -o-

c) vishazi rejeshi vyenye kiambishi rejeshi tamati -o.

Vishazi hivi hutofautiana tu kimuundo. Vishazi hivi huwasilisha wazo sawa ila kishazi rejeshi chenye kiambishi tamati -o ambacho huelekea kuleta wazo la mazoea. Vishazi rejeshi vyenye amba- ni vile ambavyo huundwa kwa kiwakilishi rejeshi amba-. Kwa mfano:

2. Mtoto **[ambaye atamaliza wa kwanza]** atatuzwa.

Vishazi rejeshi vyenye kiambishi awali -o- ni vile ambavyo huundwa kwa kukiweka kiambishi hiki katika kitenzi cha kishazi. Mathalan:

3. Mtoto **[atakayemaliza wa kwanza]** atatuzwa.

Vishazi rejeshi vyenye kiambishi tamati –o huundwa kwa kukichopeka kiambishi hiki mwishoni mwa kitenzi. Kwa mfano:

4. Mtoto **[amalizaye wa kwanza]** hutuzwa.

Vishazi rejeshi vina uamilifu wa kuvumisha. Hii ndiyo sababu wataalamu wengine huviita vishazi vumishi. Vishazi hivi hutokea baada ya nomino na humilikiwa na KN. Vinaweza kupatikana katika nafasi ya kiima ama ya yambwa. Kwa mfano:

5. a) Mti **[ambao ulianguka]** umeondolewa.

   b) Juma amevunja kiti **[kilichonunuliwa dukani]**.

Vishazi nomino rejeshi vina muundo sawa na ule wa vishazi rejeshi. Tofauti iliyopo ni kuwa vishazi nomino rejeshi vinapotumiwa haviandamani na nomino. Kwa mfano:

6. a) **[Atakayefika kwanza]** atafungulia wengine mlango.

   b) **[Aliyekupa wewe kiti** ]ndiye **[aliyenipa mimi kumbi].**

   c) **[Aliye na macho]** haambiwi tazama.

Vishazi nomino rejeshi vinaweza kubadilishana nafasi na nomino ama virai nomino. Mathalan,

7. **a) [Atakayefika kwanza]** atawafungulia wengine mlango.

   **b) [Hadija]** atawafungulia wengine mlango.

Vishazi nomino rejeshi havina uamilifu wa kuvumisha bali hurejelea nomino inayozungumziwa katika sentensi. Vishazi nomino rejeshi, tofauti na vishazi nomino vingine vya Kiswahili Sanifu vinakaribiana sana na virai nomino kwani tofauti na vishazi

nomino vingine, hurejelea sio tu dhana za kidhahania bali pia dhana halisi. Tutaona baadaye (tazama sehemu 3.4) jinsi sifa hii inavyoathiri kishazi nomino rejeshi.

### 3.1.2 Kishazi Nomino Kisoukomo

Kishazi kisoukomo cha Kiswahili Sanifu huweza kudhihirika katika miundo mbalimbali ya sentensi. Uamilifu wake hubadilika kutegemea miundo hiyo. Kwa kuwa utafiti wetu unajishughuliisha na vishazi nomino, hatutayaingilia majukumu mengine ya vishazi visoukomo bali tutaangazia vishazi nomino visoukomo tu.

Kishazi nomino kisoukomo ni kishazi ambacho hudhihirishwa na kitenzi kisoukomo. Kitenzi hiki kama tulivyotaja katika sura ya 2, hakichukui viambishi vya kiima wala vya njeo/hali. Katika Kiswahili Sanifu, kitenzi kisoukomo hudhihirishwa kwa kuchukua kiambishi kisoukomo **KU-** na mara nyingine kiambishi cha yambwa. Kwa mfano:

8. a) Ali anataka **[kula maembe yote].**

   b) Ali anataka **[kuyala maembe yote].**

Katika sentensi hizi, maneno yaliyotiwa katika mabano ndiyo yanayowakilisha kishazi nomino kisoukomo.

Ikumbukwe kwamba kiambishi hiki pia hutumiwa kuunda kitenzi – nomino ambacho hupatikana katika ngeli ya 15. Kwa kuwa utafiti huu unashughulikia kategoria za kiuamilifu wala si za kileksika, tutachukulia kwamba vitenzi ambavyo vina kiambishi awali **KU-** ni vitenzi visoukomo ambavyo kwa mujibu wa utafiti huu ndivyo vitambulishi vya kishazi nomino kisoukomo. Kwa hivyo, tutachukulia kwamba kitenzi – nomino ni

kitenzi kisoukomo ambacho kina uamilifu wa nomino katika sentensi na hivyo ni kitambulishi cha kishazi nomino kisoukomo. Kwa mfano:

9. **[Kutangulia]** si **[kufika]**.

Kishazi nomino kisoukomo mara nyingine huitwa kishazi jalizi hasa kutokana na sifa yake ya kujaliza vitenzi katika sentensi za Kiswahili Sanifu. Kwa mfano:

10. Musa anapenda **[kucheza mpira]**.

Kitenzi *anapenda* katika (10) kinahitaji kijalizo ili kiweze kukamilika. Kijalizo hiki mara nyingi huweza kuwa aidha nomino, kirai nomino au kishazi nomino. Mathalan:

11. a) Musa anapenda [**Maria]**

b) Musa anapenda **[wasichana wembamba]**.

c) Musa anapenda **[kucheza mpira]**.

Kutokana na mifano hii pia tunaweza kuona kwamba kishazi nomino kisoukomo kinaweza kubadilishana nafasi na kirai nomino katika sentensi. Sifa hii inatudhihirishia kwamba kishazi nomino kisoukomo ni kishazi nomino kwa mujibu wa maelezo tuliyotoa awali.

### 3.1.3 Kishazi Nomino 'Kwamba'

Kishazi nomino 'kwamba' ni kishazi ambacho hutambulishwa na matumizi ya kijalizi **kwamba** na mara nyingine **kuwa**. Vijalizi hivi vinapotokea katika sentensi hufuatwa na kishazi. Mathalan:

12. Mwalimu alisema **[kwamba atachelewa kidogo leo]**.

Kama tunavyoona katika sentensi hii, maneno yaliyowekwa katika mabano ni kishazi nomino 'kwamba' na yanarejelea alichosema mwalimu. Kijalizi **kwamba** ndicho kinachowasilisha kishazi hiki. Matumizi ya **kwamba** na **kuwa** hutegemea uchaguzi wa mtumiaji lugha.

Vishazi hivi mara nyingi huainishwa katika kategoria ya vishazi jalizi kwa sababu ni tungo zenye muundo wa kujaliza. Hata hivyo, ni vishazi nomino kwa sababu licha ya kuwa na sifa ya kujaliza, pia huweza kuchukua majukumu mengine ya kirai nomino katika sentensi kama katika sentensi zifuatazo:

13. a) **[Kwamba walishinda uchaguzi uliopita]** ni jambo linalojulikana wazi.

    b) Kamau alituhakikishia **[kwamba atamwoa Wanjiku]**.

Kimuundo, vishazi hivi vyaweza kuwa na kiima wazi au kisicho wazi. Tazama mifano ifuatayo:

14. a) Watumishi wanadai **[kwamba *mishahara yao* yahitaji kuongezwa]**.

    b) Mwalimu alisema **[kuwa atachelewa]**.

Katika mfano wa (14a) kiima cha kishazi nomino ni wazi yaani ***mishahara yao*** ilhali katika (14b) kiima cha kishazi nomino hakidhihiriki wazi bali kinabainishwa na kiambishi cha upatanishi ngeli katika kitenzi ***atachelewa***.

Kijalizi **kwamba** mara nyingine huweza kudondolewa hasa kinapotumiwa katika nafasi ya yambwa. Kwa mfano:

15. a) Makau aliahidi **[kwamba atarejea mapema. ]**

b) Makau aliahidi **[atarejea mapema.]**

Kishazi hiki kinapotumiwa katika nafasi ya kiima hakiwezi kudondolewa bila kupoteza maana inayokusudiwa. Mathalan:

16. a) **[Kwamba watafika leo]** ni wazi.

b) * **[Watafika leo]** ni wazi.

Sentensi (16b) si sahihi kwani kijalizi **kwamba** kimedondolewa. Kwa hiyo, kishazi nomino 'kwamba' kinapotumiwa katika nafasi ya yambwa, kijalizi chake kinaweza kudondolewa bila kubadilisha maana.

Hebu tutathmini uwezo wa aina hizi tatu za vishazi nomino wa kuchukua nafasi za virai nomino.

## 3.2 NAFASI ZA AGIUMENTI KATIKA KISWAHILI SANIFU

Katika sehemu hii tumetathmini uwezekano wa vishazi nomino kuchukua nafasi za virai nomino. Kwanza, tumeufafanua muundo wa agiumenti wa kitenzi cha Kiswahili Sanifu na kuzitambua nafasi za agiumenti zinazoteuliwa na vitenzi vya Kiswahili Sanifu. Ufafanuzi huu umetuongoza katika kutathmini uwezekano wa vishazi nomino kuchukua nafasi za virai nomino kisemantiki.

Kwa mujibu wa Radford (1997:324), kila sentensi sahili ina kiarifu na kundi la agiumenti. Kiarifu ni kipashio cha kileksika ambacho hueleza uhusiano fulani baina ya vipashio ilhali agiumenti ni vipashio vinavyohusishwa na kiarifu. Kiarifu chaweza kuwa ni kitenzi, kivumishi, kihusishi au hata jina. (Tumeshugulikia kiarifu kama kitenzi tu ili tuweze kujikita katika mipaka ya utafiti huu). Nafasi ya agiumenti huchukuliwa na

nomino au virai nomino katika sentensi. Kiarifu huweza kuamua idadi ya agiumenti kitakazoteua. Idadi ya agiumenti inayoteuliwa na kiarifu ndiyo hutuwezesha kujua muundo wa agiumenti wa kiarifu husika. Hebu tuangalie sentensi ifuatayo:

17. **[Juma]** alimpiga **[Maria]**.

Katika sentensi (17) kitenzi ***alimpiga*** kinajumuisha washiriki wawili: anayetenda na anayeathiriwa na kitendo. Kwa hivyo, ***Juma*** ndiye mwenye kutenda kitendo naye tutamwita **Mtenda**. ***Maria*** ndiye mwenye kuathiriwa na kitendo naye ataitwa **Mtendwa**.

Kitenzi hiki kina muundo ufuatao:

18. piga; kitenzi [ (x) (y) ]
mtenda mtendwa

Katika Kiswahili Sanifu kitenzi elekezi kama ***piga*** kitachukua agiumenti mbili – mtenda na mtendwa.

Kunavyo vitenzi vingine ambavyo huchukua zaidi ya agiumenti mbili kama katika sentensi ifuatayo:

19. **[Wakaazi wa Embakasi]** watampigia **[Esther Passaris][kura]**.

Katika sentensi (19) kitenzi ***pigia*** kina agiumenti tatu ambazo ni ***Wakaazi wa Embakasi*** ambayo ni mtenda, ***Esther Passaris*** ambayo ni **mtendewa** na ***kura*** ambayo ni mtendwa. **Mtendewa** ni nafasi inayochukuliwa na jina linalofaidika kutokana na kitenzi. Mara nyingi, nafasi ya mtendewa huamuliwa na kitenzi kilichonyambuliwa katika kauli ya kutendea.

Kitenzi hiki hivyo kitakuwa na muundo wa agiumenti ufuatao:

20. pigia: kitenzi [ (x) (y z) ]
mtenda mtendewa mtendwa

Vitenzi vya Kiswahili Sanifu pia huweza kuchukua agiumenti moja tu. Mathalan:

21. **[Watu wote]** walishangaa sana.

Katika sentensi (21) kitenzi *shangaa* kinachukua agiumenti moja tu nayo ni ya mtenda yaani ***watu wote.*** Vitenzi vya aina hii mara nyingine huitwa vitenzi visoelekezi kwani havichukui yambwa. Mathalan, hatuwezi kusema **Watu wote walishangaa Maria.* Vitenzi hivi, hata hivyo, huweza kuchukua vielezi. Kitenzi hiki kina muundo wa agiumenti ufuataao:

22. shangaa: kitenzi [ (x) ]
mtenda

Kunavyo vitenzi vingine ambavyo hueleza hali fulani kama katika sentensi zifuatazo:

23. **a) [Juma]** alikufa.

**b) [Karisa]** anampenda **[Lulu]**.

Katika sentensi (23a), ***Juma*** si mtenda kwani siye anayesababisha kitendo ***Kufa***; kinatokea tu. *Karisa* naye, katika (23b), siye anayesababisha kitendo '***penda***'. Kwa hakika anaweza kumpenda Lulu tu bila kutia juhudi yoyote. Kwa sababu hii nafasi ya *Juma* na *Karisa* si ya mtenda bali ni ya **Mwathiriwa**. **Mwathiriwa** ni nafasi inayochukuliwa na nomino inayoathiriwa na hali fulani. Mwathiriwa hasababishi kitendo kinachozungumziwa na kitenzi.

Katika (23b), nafasi inayochukuliwa na *Lulu* si ya mtendwa kwani kitendo ***penda*** hakimfanyii chochote kinachomwathiri kwa uwazi kama ilivyo katika (17) ambapo Maria anaathiriwa kwa uwazi na kitendo ***piga***. Kwa hivyo nafasi inayochukuliwa na *Lulu* si ya

mtendwa bali ni **Mrejelewa**. **Mrejelewa** ni nafasi ambayo huteuliwa na kitenzi elekezi. Hivyo kitenzi ***penda*** kitakuwa na muundo wa agiumenti ufuatao:

24. penda: kitenzi [ (x) (y) ]
Mwathiriwa Mrejelewa

Kunazo nafasi nyingine za agiumenti zinazoweza kubainishwa kama vile kifaa, lengo, chanzo, mahali na kadhalika ila tutazishughulikia hizi tu kwani ndizo zinazotusaidia kuendeleza mada yetu. Nafasi za agiumenti huamuliwa na vitenzi halisi. Vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi haviteui nafasi za agiumenti. Hata hivyo, vitenzi hivi vinaweza kuwa vinahitaji kiima na yambwa. Nafasi hizi tutaziita nafasi zisizo za agiumenti kisha tumethmini uwezo wa vishazi nomino wa kuchukua nafasi zisizo za agiumenti katika sehemu 3.5.

## 3.3 VISHAZI NOMINO VYA KISWAHILI SANIFU KATIKA NAFASI ZA AGIUMENTI

Katika sehemu hii tumetathmini uwezekano wa vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu kuchukua nafasi za agiumenti tulizotambulisha katika sehemu 3.3. Tumezishughulikia nafasi hizi za agiumenti kimuundo katika sehemu hii. Hata hivyo, ni muhimu kutaja kuwa nafasi hizi za agiumenti zinaweza kuchukua nafasi mbalimbali kimuundo bila kubadilika. Mathalan:

25. a) Juma alimpiga Maria.

b) Maria alipigwa na Juma.

Katika (25a), *Juma* ni kiima na ni mtenda ilhali *Maria* ni yambwa na ni mtendwa. Hata hivyo katika (25b), **Maria** ni mtendwa lakini ni kiima si yambwa tena. Tunaona kwamba

*Juma*, ingawa bado ni nafasi ya agiumenti, inateuliwa na kihusishi *na*. Kwa hivyo, kwa madhumuni ya kujikita katika upeo na mipaka ya utafiti huu, hatujayaingilia haya.

Kwa kuwa nafasi za agiumenti huchukuliwa na nomino ama virai nomino, tutatumia nadharia ya uminimalisti kukagua uhusika wa vishazi nomino hivi katika nafasi ya spesifaya ya ama kiima au yambwa ambapo virai nomino hukaguliwa uhusika ili kuthibitisha uwezekano huu.

### 3.3.1. Mtenda

Hii ni agiumenti ambayo huamuliwa na takribani vitenzi vyote vinavyoweza kuamua nafasi za agiumenti. Hii ni nafasi ambayo kisintaksia huchukuliwa na kiima. Hebu tutazame sentensi zifuatazo:


26. a) [ **Rais huyu mpya** ] atabadilisha sera za nchi.

    b) [ **Atakayechaguliwa mwaka huu** ] atabadilisha sera za nchi.

Katika (26) kitenzi ***badilisha*** kinateua nafasi ya mtenda ambayo katika (26a) inachukuliwa na kirai nomino ***Rais huyu mpya*** na katika (26b) inachukuliwa na kishazi nomino rejeshi ***Atakayechaguliwa mwaka huu***. Kwa kuwa nafasi ya mtenda huelekea kuchukuliwa na nomino inayosababisha kitendo kwa hiari, nomino hii mara nyingi huwa ni nomino hisivu. Kwa hivyo tunaona kwamba nafasi hii huweza tu kuchukuliwa na KN au kishazi nomino rejeshi tu kwani ndicho kina sifa ya kuwakilisha vitu halisi na vya


dhahania[7]. Nafasi hii ya mtenda itakaguliwa sifa katika nafasi ya kiima kama katika michoro ifuatayo:

27. a) **[Rais huyu mpya]** atabadilisha sera za nchi.




[7] Kishazi nomino kisoukomo huweza kutokea katika nafasi hii lakini kwa kuwa hakiwakilishi nomino halisi hakiwezi kuitwa mtenda ingawa kinaelekea kuamuliwa nafasi ya mtenda na kitenzi husika. Kwa mfano: **Kuchaguliwa kwake mwaka huu** kutabadilisha sera za nchi.
Kitenzi ***badilisha*** kinateua kishazi nomino (kilichokolezwa rangi) katika nafasi ya mtenda lakini kutokana na umilisi wa mwanalugha ni wazi kwamba kishazi nomino kisoukomo, ingawa kinachukua nafasi ya mtenda, hakitoshelezi maelezo ya mtenda. Hii basi tutaichukulia kuwa si nafasi ya agiumenti.

b) **[Atakayechaguliwa mwaka huu]** atabadilisha sera za nchi.




Kama tunavyoona katika michoro hii (27a) na (27b), kirai nomino na kishazi nomino rejeshi vinakaguliwa uhusika katika nafasi ya spesifaya ya kiima. Jambo hili linatudhihirishia kwamba kirai nomino rejeshi kinaweza kuchukua nafasi ya kirai nomino.

### 3.3.2. Mtendwa

Nafasi hii ya agiumenti huchukuliwa na nomino inayopata athari ya kitendo kinachosababishwa na mtenda. Nafasi hii ya mtendwa huteuliwa hasa na vitenzi tendi ambavyo mara nyingi athari yake hubainika wazi. Nafasi hii kisintaksia huchukuliwa na yambwa. Tuangalie sentensi zifuatazo:

28. a) Yohana alimpiga **[Mary]**.


    b) Yohana alimpiga **[aliyemkasirisha]**.

Katika sentensi hizi, kitenzi ***piga*** ni kitenzi elekezi ambacho kinateua agiumenti mbili – mtenda na mtendwa. Kitenzi hiki kina muundo ufuatao;


29. piga: kitenzi ( KN  KN/S)

Hivi ni kusema kwamba agiumenti ya mtendwa yaweza kuwa ni KN ama ni kishazi kama katika (28b). Kwa mujibu wa Haegmann (1994) kitenzi huwa na muundo wa agiumenti ambao unakiwezesha kuchagua idadi ya agiumenti wala si aina ya agiumenti. Kwa hivyo kitenzi kinaweza kuteua agiumenti mbili au hata tatu lakini hakiamui agiumenti hizo zitakuwa ni KN ama ni kishazi nomino. Katika kukaguliwa uhusika, nafasi ya mtendwa itakaguliwa katika nafasi ya spesifaya ya yambwa. Mathalan:

30. a) Yohana alimpiga [Maria].




b) Yohana alimpiga [aliyemkasirisha].



### 3.3.3. Mwathiriwa

Nafasi ya mwathiriwa huchukuliwa na nomino inayoathiriwa na hali fulani. Vitenzi hivi vyaweza kuwa vitenzi elekezi au visoelekezi. Kwa mfano:

31. a) **[Musa ]** alifariki jana.


    b) **[Walionusurika ]** walifariki jana jioni.

Kitenzi ***fariki*** kina muundo wa agiumenti unaoweza kuchukua ama KN au kishazi nomino rejeshi.

32. fariki: kitenzi ( KN/S )

Kama inavyobainika katika (31), hii ni nafasi ya kiima na hivyo itakaguliwa katika nafasi ya spesifaya ya kiima. Tazama mchoro ufuatao:

33. **[Walionusurika]** walifariki jana jioni.



### 3.3.4 Mrejelewa

Vitenzi elekezi vya Kiswahili Sanifu huweza kuteua nafasi mbili za agiumenti. Hata hivyo, nafasi ya agiumenti inayoteuliwa hutegemea maana ya kisemantiki ya kitenzi. Nafasi ya mrejelewa huteuliwa na vitenzi tambuzi, vitenzi vya fahamu au pia vitenzi vya hisia. Matahalan;

35. a) Mkurugenzi ameahidi **[nyongeza ya mshahara]**.

b) Mkurugenzi amewaahidi **[walichotaka]**.

c) Mkurugenzi ameahidi **[kuwapa wafanyakazi marupurupu yao]**.


d) Mkurugenzi ameahidi **[kwamba atazungumza nao leo]**.

Kitenzi *ameahidi* kinaweza kuteua nafasi mbili za agiumenti kama inavyobainika katika (35). Nafasi ya mrejelewa, ambayo ndiyo iliyokolezwa rangi, inaweza kuchukuliwa na KN kama katika (35a) ama kishazi nomino kama katika (35b – d).

Tofauti na nafasi ya mtendwa, nafasi ya mrejelewa inaweza kuchukua aina zote tatu za vishazi nomino. Hii ni kwa sababu agiumenti katika nafasi hii zaweza kuwa ni halisi au za dhahania. Vitenzi vinavyoteua nafasi hii ya mrejelewa huweza kujalizwa na nomino za dhahania ama halisi tofauti na vitenzi vya kutenda ambavyo hujalizwa na nomino halisi.

Kimuundo, nafasi ya mrejelewa huweza kuwa ni nafasi ya yambwa na hivyo katika michoro, nomino katika nafasi hii hukaguliwa uhusika katika nafasi ya yambwa. Tazama mchoro huu:

36. Mkurugenzi ameahidi **[kuwapa wafanyakazi marupurupu yao.]**




## 3.3.5. Mtendewa

Vitenzi vya Kiswahili Sanifu vinaponyambuliwa katika kauli ya kutendea, hukipa kitenzi uwezo wa kuteua agiumenti ya mtendewa juu ya ile ya mtenda na mtendwa. Nafasi ya agiumenti ya mtendewa huchukuliwa na nomino inayofaidi kutokana na kitendo kile. Kwa mfano:

37. a) Ali alimnunulia **[Hadija]** maua.


b) Ali alimnunulia **[ampendaye]** maua.

Kutokana na mfano huu tunaona kuwa kitenzi ***nunulia*** kinaweza kuchukua agiumenti tatu na agiumenti ya mtendewa inaweza kuwa aidha ni kirai nomino ama ni kishazi nomino rejeshi kama katika (37b). Hivyo muundo wa agiumenti wa kitenzi hiki ni:

38. nunulia: kitenzi (KN KN/S KN)

Katika kukagua uhusika, itabidi tutengeneze kifundo cha kirai cha mtendewa na kukagua sifa katika nafasi ya spesifaya ya kirai hiki. Ikumbukwe kwamba kwa mujibu wa nadharia ya uminimalisti, vifundo hutengenezwa kutegemea ushahidi wa leksika ama sintaksia. Tazama mchoro fuatao:

39. Ali alimnunulia **[ampendaye]** maua.



Ni muhimu kutaja kuwa kuna uwezekano wa baadhi ya vitenzi kuchukua vishazi nomino katika nafasi zote za agiumenti. Vishazi nomino vinapotokea katika nafasi zote za agiumenti katika sentensi moja, maana ya sentensi hufichika zaidi hivi kwamba muktadha unahitajika sana ili kuelewa ujumbe wa sentensi. Mathalan:

40. a)**[Waliopewa kandarasi hiyo]** waliwahamisha **[waliokuwa wakiishi hapo]**.

b) **[Waliotumwa]** walimpelekea **[aliyekuwako]** **[alichoahidiwa]**.

Kama inavyobainika katika sehemu hii, nafasi za agiumenti za mtenda, mtendwa, mwathiriwa na mtendewa zinaelekea kuchukuliwa tu na vishazi nomino rejeshi si vishazi vinginevyo hasa kwa sababu nafasi hizi huchukuliwa na nomino halisi. Kama tulivyotangulia kutaja hapo awali, ni vishazi nomino rejeshi tu ambavyo vinaweza kurejelea dhana halisi na dhahania pamoja. Hii ndiyo sababu inayofanya vishazi nomino vingine visiweze kuchukua nafasi hizi za agiumenti. Hata hivyo nafasi ya agiumenti ya mrejelewa inaweza kuchukuliwa na aina zote tatu za vishazi nomino kwa sababu inaweza kurejelea dhana dhahania.

## 3.4 VISHAZI NOMINO VYA KISWAHILI SANIFU KATIKA NAFASI ZISIZO ZA AGIUMENTI

Vishazi nomino huweza kuchukua nafasi zisizo za agiumenti. Hizi ni nafasi ambazo huweza kujibainisha kisintaksia tu wala haziwezi kuteuliwa nafasi za agiumenti kisemantiki na vitenzi kama tulivyofafanua katika 3.3. Kama tulivyotangulia kueleza katika 3.3, vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi haviteui nafasi za agiumenti. Hata hivyo, ni wazi kwamba vitenzi hivi huhitaji vijalizi ambavyo mara nyingi huwa ni virai

nomino. Katika sehemu hii, tumetathmini uwezekano wa vishazi nomino kuchukua nafasi zisizo za agiumenti.

### 3.4.1 Kiima

Hii ni nafasi ambayo mara nyingi huchukuliwa na KN na ndiyo huelezwa na kitenzi. Kiima huweza kutokea na aina zote za vitenzi. Hata hivyo, tumejishughulisha na kiima katika tungo zenye vitenzi vishirikishi na vitenzi visaidizi pekee kwani tumekwisha ishughulikia nafasi hii ya kiima kama nafasi ya agiumenti katika 3.4. Katika sehemu hii tumeishughulikia kama nafasi isiyo ya agiumenti. Katika Kiswahili Sanifu, kiima hutangulia kitenzi. Tazama sentensi zifuatazo:

41. a) **[Cynthia]** ni msichana mzuri.

 b) **[Kumjibu mwalimu hivyo]** ni dharau kwake.

 c) **[Waliotutembelea jana]** ni wagonjwa.

 d) **[Kwamba itanyesha leo]** ni dhahiri.

Maneno yaliyotiwa katika mabano katika (41) yanachukua nafasi ya kiima katika sentensi hizo. Nafasi hii huchukuliwa na KN kama katika (41a) au kishazi nomino kama inavyodhihirika katika (41b - d). Kama tunavyoona, vishazi nomino vyote vinaweza kuchukua nafasi hii ya kiima hasa vinapotumiwa na kitenzi kishirikishi. Vitenzi visaidizi vinapotumiwa, kishazi nomino cha kwamba hakiwezi kutumika katika nafasi ya kiima. Tazama mifano ifuatayo:


42. a) **[Kutembea usiku]** kumekwisha pigwa marufuku.

 b)[ **Yaliyonunuliwa jana]** yalikuwa yameharibika.


 c) *[**Kwamba utachelewa**] ulikuwa umejua.

Katika kukagua uhusika wa vishazi nomino katika nafasi ya kiima, vishazi nomino husogezwa na kukaguliwa uhusika wake katika nafasi ya spesifaya ya kirai cha upatanisho wa kiima. Tazama mifano ifuatayo:

43. a) Cynthia ni msichana mzuri.



b) Kumjibu mwalimu hivyo ni dharau.




Kama tunavyoona katika michoro hii, KN, *Cynthia*, katika 43a na kishazi nomino, *kumjibu mwalimu hivyo*, katika 43b zinakaguliwa uhusika katika nafasi ya kiima. Hili ni thibitisho kuwa kishazi nomino katika sentensi hizi kina jukumu sawa na la KN.

### 3.4.2 Kijalizo Cha Kiima

Kijalizo cha kiima hupatikana na vitenzi vishirikishi tu. Kijalizo cha kiima huweza aidha kueleza sifa za kiima ama kukitambulisha kiima chenywe. Kimuundo, kijalizo cha kiima hutokea mara tu baada ya kitenzi. Kijalizo cha kiima hudhihirishwa na KN, KV, KH, KE ama na kishazi nomino. Kwa mfano:

44. a) Aliyefika kwetu asubuhi ni **[Juma]**. (KN)

b) Juma ni **[mzuri]**. (KV)

c) Ndege wengi wako **[juu ya miti hii].** (KH)

d) Wanafunzi wako **[darasani]**. (KE)

e) Mkurugenzi huyu mpya ndiye **[aliyeniachisha kazi]**. (Kishazi nomino rejeshi)

Nafasi hii ya kijalizo cha kiima huweza kuchukuliwa na vishazi nomino vya aina zote tatu kama inavyobainika katika 45.


45. a) Alichoniambia ni **[kwamba atachelewa kufika kazini leo**].

b) Jambo linalomsikitisha Mary ni **[kumpigia kelele kila siku]**.

c) Mwalimu huyu ndiye **[aliyetufunza kusoma na kuandika]**.

Uhusika wa vishazi nomino hukaguliwa katika nafasi ya kijalizo cha kiima. Kifundo cha kijalizo cha kiima kitatengenezwa na vishazi nomino kukaguliwa uhusika wake katika nafasi ya spesifaya ya kijalizo cha kiima. Kwa mfano:

46. a) Alichoniambia ni [kwamba atachelewa kufika kazini leo].




## 3.4.3. Kijalizo Cha Kivumishi

Katika sura ya 2 tulitaja kwamba kuna vivumishi vya aina mbalimbali. Mojawapo ya aina hii ya vivumishi ni vivumishi vya a – unganifu. Vivumishi hivi huhitaji kijalizi ili viweze kukamilika. Nafasi hii ya kijalizo huchukuliwa mara nyingi na KN. Hata hiyvo, nafasi hii pia huweza kuchukuliwa na kishazi nomino. Kwa mfano:

47. a) Wanafunzi wa **[shule jirani]** wametoroka.

b) Arusi ya **[kufana sana]** ilifanywa jana.

c) Mazishi ya **[aliyekuwa mbunge wa Karisma]** yameahirishwa.

Katika (47a), kijalizo cha kivumishi ni KN ilhali katika (47b na c) ni kishazi nomino kisoukomo na kishazi nomino rejeshi mtawalia. Kama tunavyoona kishazi nomino cha kwamba hakiwezi kutumika katika nafasi hii. Mathalan:

48. * Maonyesho ya **[kwamba atafika]** yalifana sana.

Hivyo, nafasi ya kijalizo cha kivumishi cha a-unganifu huchukuliwa na kishazi nomino kisoukomo ama na kishazi nomino rejeshi.

Kivumishi cha pekee –enye pia ni kivumishi ambacho huhitaji kijalizo. Mara nyingi kijalizo cha kivumishi hiki kama kile cha a–unganifu huwa ni KN ama kishazi nomino. Kishazi nomino kinachotumiwa kujaliza kivumishi cha – enye ni kishazi kisoukomo pekee. Kwa mfano:

49. a) Mtu mwenye **[kofia nyeusi**] amepita hapa.


b) Mtu mwenye **[kutembea kwa haraka]** hufika haraka.

Kishazi nomino rejeshi na kishazi nomino cha kwamba haviwezi kutumiwa kujaliza kivumishi cha –enye. Kishazi nomino rejeshi hakiwezi kutumika kujaliza kivumishi cha -enye kwa sababu kiwakilishi rejeshi amba- na –o– rejeshi hutumiwa kuleta maana sawa na ile inayotolewa na kivumishi –enye. Kwa hivyo kutumiwa pamoja kutasababisha kujirudia ovyo na kukosa usarufi. Kwa mfano:

50. * Mtu mwenye **[anayetembea haraka**] hufika haraka.

Kijalizo cha kivumishi hutokea ndani ya KV ambavyo hutokea katika nafasi ya kiima au ya yambwa. Tazama michoro ifuatayo:


51. a) Mtu mwenye [kutembea kwa haraka] hufika haraka.




* Hiki ni kishazi kisoukomo ambacho kimetumiwa kujaliza kivumishi –enye.

Tazama kinavyowasilishwa katika mchoro 51b.

51. b) Kutembea kwa haraka



### 3.4.4 Kijalizo Cha Kihusishi

Virai husishi mara nyingi kama tulivyotangulia kutaja katika sura ya 2, huhitaji kujalizwa kwa KN. Nafasi hii ya kijalizo cha kirai husishi pia huweza kuchukuliwa na kishazi nomino. Mathalan:

52. a) Paula aliondoka baada ya **[chakula cha mchana]**.

b) Alitaaabika kwa **[kutotilia maanani mawaidha ya mamake]**.


c) Kabla ya **[waliotarajiwa kuondoka]**, wapeni chakula.

Katika (52) vihusishi *baada ya, kwa* na *kabla ya* vinajalizwa na KN, kishazi nomino kisoukomo na kishazi nomino rejeshi mtawalia. Kishazi nomino cha kwamba hakiwezi kuchukua nafasi hii ya kijalizo cha kihusishi. Tazama mfano huu:


53. * Nitaondoka baada ya **[kwamba nimemjulisha]**.

Kijalizo cha kihusishi ni kiambajengo cha kirai husishi. Kwa hivyo, katika michoro kitatokea pale kirai husishi kitakapotokea. Kwa mfano:

54. a) Alitaabika kwa [kutozingatia mawaidha ya mamake].



55. b) Kutozingatia mawaidha ya mamake. *




### 3.4.5. Kijalizo cha nomino

Kishazi nomino wakati mwingine huweza kutumika kujaliza nomino. Mathalan:


55. Fununu **[kwamba uchaguzi utachelewwa]** zilienea nchini kote.

56. Wakurugenzi wa kampuni walikutana kujadili ripoti **[kwamba kampuni yao ilifilisika]**.


Katika sentensi hizi, vishazi nomino vimekolezwa rangi. Vishazi nomino hivi vinajaliza nomino zinazovitangulia. Katika (55) kishazi nomino ***kwamba uchaguzi utachelewa*** kinajaliza jina ***fununu*** na katika (56) kishazi nomino ***kwamba kampuni yao ilifilisika*** kinajaliza jina ripoti.

Vishazi nomino hivi hupatikana katika KN ambacho chaweza kutokea katika sentensi kama kiima ama yambwa kama inavyobainika katika mchoro ufuatao:

57. a) Fununu **[kwamba uchaguzi utachelewa]** zilienea nchini kote




58. b) kwamba uchaguzi utachelewa*



## 3.5 HITIMISHO

Katika sura hii tumeainisha vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu kisha tukatathmini uamilifu wake katika nafasi za virai nomino kisemantiki na kisintaksia. Kama tulivyoona kutokana na data tuliyotumia, vishazi nomino vinaweza kuchukua nafasi za virai nomino ila vimebanwa kwa kiasi fulani kuliko virai nomino. Vishazi nomino vinaweza kuwa na uamilifu sawa na wa virai nomino lakini havina uhuru mwingi kama wa virai nomino hasa kutokana na muundo wake na matumizi yake. Kutokana na utafiti wetu, tumebainisha kwamba vishazi nomino huchaguliwa na kuthibitiwa na vitenzi, vivumishi, nomino na hata vihusishi. Kwa hivyo, tunaona kwamba kuna vishazi nomino vinavyoweza kutumiwa na baadhi ya maneno na si mengine. Katika sura inayofuata tumetathmini upatanisho wa kisarufi baina ya kishazi nomino na kishazi kikuu.

# SURA YA NNE

# RUWAZA YA UPATANISHO WA KISHAZI NOMINO

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura ya 3 tuliviainisha vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu na kutathmini uamilifu wake katika sentensi. Katika sura hii tutajishughulisha na ruwaza ya upatanisho wa kishazi nomino na kishazi kikuu. Kwa kuwa kishazi nomino ni kishazi bebwa, uhusiano wake na wa kishazi kikuu ni uhusiano wa kiutegemezi. Kwa hivyo, tumetathmini kama kishazi kikuu kinaathiri au kuathiriwa kiupatanishi na kishazi nomino.

## 4.1 RUWAZA YA UPATANISHO KATIKA KISWAHILI SANIFU

Kiswahili ni lugha ambishibainishi. Kwa hivyo, kuna mwingiliano mkubwa wa mofolojia yake na sintaksia yake. Mwingiliano huu hubainika wazi hasa katika upatanisho wa kisarufi. Upatanisho huu huathiriwa na nomino. Nomino ndizo msingi wa upatanisho katika sentensi kwani ndizo huamua ruwaza ya upatanisho. Nomino za Kiswahili Sanifu zimeambishiwa viambishi vya upatanisho wa ngeli (tazama sura 2 sehemu 2.2.1). Nomino hizi hukubaliana kiidadi na katika ngeli na vipengele vingine katika sentensi yaani vitenzi, vivumishi na viwakilishi. Kubadilika kwa jina husababisha kubadilika kwa upatanisho huu. Kwa mfano:

1. Mutiso **a**me**mw**oa Maria, msichana amba**ye** **a**li**m**penda tangu **wa**liposafiri pamoja katika gari **li**li**lo**pata ajali, na **wa**kaenda Mombasa.

Katika sentensi 1, viambishi vya upatanisho vinabadilika kulingana na ngeli za nomino zinazorejelewa. Upatanisho katika sentensi hutegemea sana KN katika sentensi. Wazo hili linathibitishwa na Vitale (1981:13) ambaye anasema kwamba utaratibu wa upatanisho wa lugha za kibantu na Kiswahili Sanifu hasa huwa ni baina ya KN kikuu na kitenzi pamoja na vivumishi na makundi mengine ya kileksika.

Upatanisho katika Kiswahili Sanifu pia huashiriwa na viambishi vya nafsi. Viwakilishi vya nafsi huhitaji kubainishwa katika ngeli 1 na 2 hasa tunapozungumzia nomino zinazorejelea binadamu. Kuna nafsi tatu katika lugha ya Kiswahili Sanifu. Nafsi hizi zina viambishi tofauti. Tazama jedwali hili:

**Jedwali 1: Nafsi na viambishi katika Kiswahili**

| Nafsi | Umoja | Kiambishi | Wingi | Kiambishi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mimi | Ni- | Sisi | Tu- |
| 2 | Wewe | U- | Nyinyi/Ninyi | M- |
| 3 | Yeye | A- | Wao | Wa- |

Viambishi hivi ndivyo huashiria upatanisho wa nafsi. Kwa mfano:

2. a) **Ni**nampenda Juma sana.

   b) **U**tachelewa kama **u**taendelea kukaa hapo.

   c) **Wa**nataka kwenda kwa nyanya yao.

Viambishi vya nafsi vyaweza kutokea pamoja na viwakilishi vya nafsi vyenyewe. Katika nafasi ya yambwa, viambishi vya nafsi ndivyo huambishwa katika kitenzi. Kiwakilishi chenyewe kinapotumika katika nafasi ya yambwa huwa na nia ya kutilia mkazo.

Vitenzi vya Kiswahili Sanifu mara nyingi huchukua upatanisho wa kiima kulingana na ngeli au nafsi ya KN chake (isipokuwa kitenzi kisoukomo). Hiki mara nyingi huwa ndicho kiambishi cha kwanza (ila kunapokuwa na ukanushi). Kiambishi hiki ni cha lazima katika mofolojia ya kitenzi cha Kiswahili Sanifu.

Upatanisho pia hudhihirika katika kuonyesha uambishi wa urejeshi. Uambishi huu hudhihirika katika kitenzi. Kiambishi cha urejeshi huonyesha upatanisho na KN kinachorejelewa. Viambishi vya urejeshi ni tofauti na vya kiima ingawa pia hutegemea ngeli. Tazama jedwali lifuatalo:

**Jedwali 2: Viambishi vya urejeshi**

| Ngeli | Kiambishi cha urejeshi |
|---|---|
| 1 | -ye- |
| 2 | -o- |
| 3 | -o- |
| 4 | -yo- |
| 5 | -lo- |
| 6 | -yo- |
| 7 | -cho- |
| 8 | -vyo- |
| 9 | -yo- |
| 10 | -zo- |
| 11 | -o- |
| 14 | -o- |
| 15 | -ko- |
| 16 | -po- |
| 17 | -ko- |
| 18 | -mo- |

Mifano ya viambishi vya upatanisho katika sentensi:

3. Watu wali**o**pigiwa simu ndio wali**o**chukuliwa.
4. Nchi amba**yo** inajitegemea ndiyo huendelea.
5. Mahali ali**ko**enda hakujulikani.

Vitenzi vya Kiswahili Sanifu pia huambishiwa viambishi vya upatanisho wa yambwa tendwa au tendewa. Viambishi hivi ni sawa na vya kiima ila kile cha nafsi ya tatu umoja ambacho ni m- (mw- kabla ya irabu). Viambishi hivi hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Mathalan:

6. Wakenya wali**wa**shinda wachezaji wa Zimbabwe wiki jana.
7. Ali**ki**poteza kile kitabu ulicho**mw**azima.

Kwa mujibu wa maelezo haya, tumeweza kubainisha kwamba katika Kiswahili Sanifu upatanisho huathiriwa na ngeli ya jina kuu katika KN. Ngeli ya nomino huathiri upatanisho wa viwakailishi, vivumishi na hata vitenzi katika sentensi. Uelewa huu ndio tuliotumia katika kuukagua upatanisho baina ya kishazi nomino na kishazi kikuu katika sehemu zifuatazo.

## 4.2 UPATANISHO WA KISHAZI NOMINO REJESHI

Upatanisho katika kishazi nomino rejeshi huamuliwa na KN kinachorejelewa kama ilivyo katika kishazi rejeshi. KN husika huathiri kiambishi cha upatanisho wa kiima na kiambishi cha urejeshi na cha yambwa. Mathalan:

8. **[**A**li**ye**wa**ambia hayo] **aliwa**danganya.

Katika sentensi hii, kiambishi **a** katika ***aliwadanganya*** ni kiambishi cha upatanishi wa kiima na kinakubaliana na kiima cha sentensi hii ambacho ni kishazi nomino rejeshi kilicho katika mabano. Kiambishi **wa** kinarejelea yambwa tendwa ambalo katika sentensi hii si wazi. Kuna upatanisho katika kishazi nomino rejeshi ambao unawakilishwa na kiambishi cha kiima **a** ambacho ndicho kinachoamua upatanisho katika kitenzi cha kishazi kikuu. Mabadiliko katika kiambishi hiki cha kishazi nomino huathiri upatanisho wa kishazi kikuu. Mathalan:

9. a) [**Ki**li**cho**liwa] **ki**liwaathiri wote.

   b) [**Ya**li**yo**liwa] **ya**liwaathiri wote.

Kama tunavyoona katika sentensi 9, kiambishi cha upatanisho wa kiima katika kishazi nomino rejeshi kinakubaliana na kiambishi cha upatanisho wa kiima katika kishazi kikuu. Vile vile kiambishi cha urejeshi katika kishazi nomino rejeshi kinakubaliana katika vishazi vyote viwili. Hivyo tunaweza kusema kwamba kishazi nomino rejeshi kinapokuwa katika nafasi ya kiima ndicho huamua upatanisho wa kishazi kikuu. Hii ni kwa sababu kishazi nomino rejeshi kama tulivyotaja katika sura ya 3, huchukua nafasi ya KN.

Katika nafasi ya yambwa, upatanisho wa kishazi nomino rejeshi huathiriwa na kiima au yambwa ya kishazi kikuu. Hebu tuzikague sentensi hizi:


10. Jabali anataka **[alichomwahidi baba.]**

11. Jabali anamtaka **[aliyemchoma mtoto.]**


**12.** Jabali anayataka **[yaliyochemshwa leo.]**

Katika sentensi 10, kiima cha kishazi kikuu ndicho kinachoathiri upatanisho wa kiima cha kishazi nomino rejeshi. Kama tunavyoona, kiambishi cha kiima cha kishazi kikuu kinakubaliana na kiambishi cha upatanisho wa kiima cha kishazi nomino rejeshi. Kimantiki, sentensi hii itaeleweka kwamba aliyetoa ahadi ni *Jabali*. Utata hata hivyo, unaweza kuingia hasa tunapoiangalia sentensi ya 11, ambayo ina kiambishi cha upatanisho wa kiima cha kishazi nomino rejeshi kinachokubaliana na cha kishazi kikuu. Hakika, ingawa viambishi hivi vinakubaliana, ukweli ni kwamba kiima cha sentensi 11 hakiathiri upatanisho wa kiambishi cha kiima cha kishazi nomino rejeshi. Upatanisho unaathiriwa na yambwa ya kishazi kikuu. Utata unatokea kwa sababu inaonekana kwamba kiima cha kishazi kikuu na yambwa ya kishazi kikuu viko katika ngeli moja. Sentensi ya 12 inaonyesha kwa uwazi zaidi jinsi yambwa ya kishazi kikuu inavyoathiri upatanisho wa kiima cha kishazi nomino rejeshi. Hebu tuangalie jinsi vielelezo vya sentensi 10 na 12 vitakavyotusaidia kuielewa hoja hii vema zaidi.

13. a) Jabali anataka alichomwahidi baba.




b) alichomwahidi baba*



Katika 13a tunaona kwamba kiima cha kishazi kikuu kinakaguliwa uhusika katika nafasi ya spesifaya ya kiima kwa sababu kiima kinadhihirika wazi kinyume na ilivyo katika 13b ambapo kiima hakijadhihirika wazi[8] na hivyo hakuna nafasi ya spesifaya. Katika sentensi ya aina hii, ndipo tunapochukulia kwamba kiima cha kishazi kikuu ni sawa na kiima cha kishazi nomino na hivyo ndicho kinachoathiri upatanisho wa kiambishi cha kiima cha kishazi nomino rejeshi. Ikumbukwe kwamba utata unaweza kutokea, kama tulivyoeleza hapo juu, iwapo yambwa ya kishazi kikuu itakuwa katika ngeli moja na kiima chake. Katika sentensi ya aina hii, kiambishi cha yambwa katika kishazi kikuu, kikidhihirishwa wazi kama katika sentensi hii, hukubaliana na kiambishi cha urejeshi katika kishazi nomino rejeshi. Mathalan:

14. a) Jabali ana**ki**taka ali**cho**mwahidi baba.


b) * Jabali ana**li**taka ali**cho**mwahidi baba.

---


[8] Kishazi nomino rejeshi kwa kawaida huwa hakina kiima kilicho wazi. Hii ni kwa sababu ili kiwe kishazi nomio rejeshi hakiwezi kutumiwa pamoja na nomino kwani kikiandamana na nomino kitakuwa ni kishazi vumishi. Rejelea maelezo katika sura 3 sehemu 3.2.1.

Hebu tukitazame kielelezo cha sentensi ya 12.

15. a) Jabali anayataka yaliyochemshwa leo.




b) yaliyochemshwa leo*



Katika kielelezo hiki tunaona kwamba kishazi nomino rejeshi hakina kiima kinachodhihirka wazi na hivyo hakuna nafasi ya spesifaya ya kiima. Hata hivyo, kama tunavyoona katika 14a, kishazi kikuu kina kiambishi cha upatanisho wa yambwa [***ya***] ambacho kinakubaliana na kiambishi cha upatanisho wa kiima cha kishazi nomino rejeshi. Kwa sababu hii, basi tunaweza kusema kwamba upatanisho wa kiima cha kishazi nomino rejeshi katika sentensi hii unaamuliwa na yambwa ya kishazi kikuu.

Kishazi nomino rejeshi kinapotumiwa katika nafasi ya kijalizo cha kiima, huathiriwa upatanisho wake wa kiambishi cha urejeshi na kiima cha kishazi kikuu. Mathalan:

16. a) Jiko hili ndilo [tuli**lo**nunua Mwembe Tayari.]

b) Nyumba hii ndiyo [ili**yo**bomolewa na wafanyakazi wa manispaa].

Kwa hivyo upatanisho wake hukubaliana na kiima na kiambishi cha kitenzi cha kishazi kikuu kama inavyobainika katika mifano iliyo hapo juu. Katika 16a, kiambishi cha urejeshi [***lo***] kinakubakiana na kiima cha kishazi kikuu, *jiko*. Vivyo hivyo katika 16b ambapo kiambishi cha urejeshi katika kishazi nomino [***yo***] kinakubaliana na kiima cha kishazi kikuu, *nyumba*. Hata hivyo kama tulivyotaja hapo awali, kiima cha kishazi nomino kinaweza kuwa tofauti na kile cha kishazi kikuu (16a) ama kiima kikawa sawa na cha kishazi kikuu (16b).

Katika nafasi ya kijalizo cha kivumishi, kishazi nomino rejeshi hakiathiriwi na kishazi kikuu wala hakiathiri upatanisho wa kishazi kikuu. Badala yake huchukua upatanisho wake kutegemea jina linalorejelewa. Mathalan:

17. Sherehe za [**wa**li**o**chaguliwa mwaka jana] zitakuwa Ijumaa.

## 4.3. UPATANISHO WA KISHAZI NOMINO KISOUKOMO

Kama tulivyofafanua hapo awali, kishazi kisoukomo hakichukui kiambishi cha upatanisho wa kiima wala cha njeo/hali bali huchukua kiambishi kisoukomo **KU-** na mara nyingine kiambishi cha yambwa. Tazama sentensi zifuatazo:

18. a) Karisa alitaka [ku**mw**oa Maria].

b) Nilijaribu [ku**uv**unja mlango huo].

Vishazi nomino visoukomo katika sentensi 18 havichukui viambishi vya njeo/hali wala kiambishi cha upatanisho wa kiima bali vinachukua kiambishi cha upatanisho wa yambwa. Hata hivyo, tunaweza kueleza nafasi ya kiima katika kishazi kisoukomo kwa mujibu wa Vitale (1981:69) ambaye anasema kuwa kimsingi kiima cha kishazi bebwa huhusiana na kiima cha kishazi kikuu. Kwa hivyo, katika sentensi (18 a na b), kiima cha kishazi nomino kisoukomo, ingawa hakidhihiriki wazi, ni sawa na cha kishazi kikuu (yaani *Karisa* na *Mimi* mtawalia). Kutokana na maelezo haya tunachukulia kwamba kiima cha kishazi nomino kisoukomo hutokana na kiima cha kishazi kikuu ama yambwa yake. Kiima hiki hudhihirika katika kishazi kikuu wala si katika kishazi nomino kisoukomo. Mathalan:

19. a) Maliki alimsihi Juma [kuenda sokoni].

b) * Maliki alimsihi Juma [Juma kuenda sokoni].


Katika (19a) kiima cha kishazi nomino kisoukomo hueleweka kimantiki kwamba kinatokana na yambwa ya kishazi kikuu ambayo ni *Juma*. Hata hivyo, hakiwezi kudhihirishwa wazi katika kishazi nomino kama inavyoashiriwa katika (19b).

Kishazi nomino kisoukomo kinapotokea katika nafasi ya kiima huathiri upatanisho wa kitenzi katika kishazi kikuu. Kwa mfano:


20. [**Ku**hesabiwa vibaya kwa kura] **ku**naweza kusababisha mchafuko wa kisisasa.

Kiambishi **KU-** kinatumiwa kuleta upatanisho katika kishazi kikuu kama inavyoonekana katika mfano huu. Hili linatokea kwa urahisi hasa tukizingatia kwamba kitenzi cha kishazi nomino kisoukomo ni kitenzi - nomino ambacho kinapatikana katika ngeli ya 15. Hebu tuangalie kielelezo cha sentensi hii.

21. a) Kuhesabiwa vibaya kwa kura kulisababisha mchafuko wa kisiasa.



b) kuhesabiwa vibaya kwa kura*




Kwa mujibu wa kielelezo hiki, tunaona kwamba kitenzi kisaidizi, *kunaweza,* ndicho kinachochukua kiambishi cha upatanisho [***ku***] kinachokubaliana na upatanisho wa kiima ambacho ni kishazi nomino kisoukomo.

Katika nafasi ya yambwa, kishazi nomino kisoukomo hakiathiriwi na upatanisho wa kishazi kikuu. Hata hivyo kinapochukua yambwa, huelekea kuchukua upatanisho wa yambwa kama inavyobainika katika mifano (19a) na (19b).

## 4.4 UPATANISHO WA KISHAZI NOMINO 'KWAMBA'

Upatanisho baina ya kishazi nomino 'kwamba' na kishazi kikuu waweza ama kuathiriwa au usiathiriwe na kiima cha kishazi kikuu. Kishazi nomino 'kwamba' kinapotokea katika nafasi ya kiima, upatanisho utatokea ndani ya kishazi nomino wala hautaathiri upatanisho katika kishazi kikuu. Kwa mfano:

22. [Kwamba **a**likuwa **a**ki**wa**danganya wananchi] ni jambo liliojulikana baadaye.

Ikumbukwe kwamba matumizi ya kishazi nomino 'kwamba' katika nafasi ya kiima yamebanika sana hasa kwa sababu ya sifa ya kishazi hiki kuwa kijalizo. Kama tulivyobainisha katika Sura 3 kishazi nomino cha kwamba hutumika katika nafasi ya kiima kinapotumika na kitenzi kishirikishi cha kuwa.

Kishazi nomino cha kwamba kinapotokea katika nafasi ya yambwa huweza kuathiriwa kiupatanishi na kiima cha kishazi kikuu au kisiathiriwe. Hebu tuzikague seentensi hizi:

23. a) Shiraz ameamua [**kwamba ataendelea na kazi**].

b) Shiraz ameamua [**kwamba Maria ataendelea na kazi**].

c) Shiraz ameamua [**kwamba wataendelea na kazi**].

Katika (23a) upatanisho katika kishazi nomino cha kwamba umeathiriwa na kiima cha kishazi kikuu ambacho ni *Shiraz*. Kishazi nomino hiki hakina kiima wazi. Kwa hivyo, kwa kuwa upatanisho wa kiima cha kishazi kikuu na wa kishazi nomino unafanana, tunachukulia kwamba kiima cha kishazi nomino ni sawa na cha kishazi kikuu. Tunaweza kukiandika kishazi nomino hiki kama:

24. Shiraz ameamua kwamba (Shiraz) ataendelea na kazi.

Katika (23b), upatanisho wa kishazi nomino na wa kishazi kikuu ni tofauti kwani upatanisho wa kiima katika kishazi nomino cha kwamba unarejelea *Maria*, licha ya kuwa kiambishi kilichotumiwa kinafanana na kile kilichotumiwa katika (23a). Matumizi ya kiima kilicho wazi katika sentensi hii ni ya msingi kwani ndiyo yanayotuwezesha kuondoa utata unaoweza kuzuka. Utata huu unaweza kuondolewa pia na matumizi ya majina yaliyo katika ngeli tofauti kama inavyobainika katika (23c). Katika hali hii kiima

cha kishazi nomino kinaweza kudondoshwa bila kuleta utata. Kama tunavyoona katika mifano hii (23), upatanisho wa kishazi nomino unaweza kuathiriwa na kiima cha kishazi kikuu iwapo kiima cha kishazi kikuu na cha kishazi nomino vitakuwa sawa. La sivyo, kishazi nomino 'kwamba' hakiathiriwi na upatanisho wa kishazi kikuu.

Tazama sentensi zifuatazo:


25. a) Shiraz amesema [**umpigie simu**.]

b) Shiraz amesema [**atakupigia simu**].


Katika sentensi hizi kijalizi **kwamba** kimedondoshwa na kiima cha kishazi nomino pia si wazi. Katika (25a) tunaweza kuchukulia kwamba kiima cha kishazi nomino ni *wewe* kwa sababu kitenzi cha kishazi nomino kimechukua kiambishi cha upatanisho wa nafsi ya 2. Isitoshe, kiambishi cha yambwa tendewa **-m-** kimetumiwa katika kitenzi hiki cha kishazi nomino na kinarejelea *Shiraz*.

Katika (25b) kiima cha kishazi nomino ni sawa na kiima cha kishazi kikuu. Yambwa ya kishazi nomino tunachukulia kuwa ni *wewe* na inawakilishwa na kiambishi cha upatanisho wa yambwa **-ku-**.

26. a) Shiraz amesema umpigie simu.





b) umpigie simu*




Vielelezo hivi vinatuonyesha kwamba kishazi kikuu kina kiima kilicho wazi ambacho ni *Shiraz,* na kinakaguliwa uhusika katika nafasi ya spesifaya ya yambwa. Hata hivyo ingawa kishazi nomino cha kwamba (kielelezo 26b) hakina kiima wazi, ni wazi kwamba kiambishi chake cha upatanisho wa kiima ni tofauti na kile cha kishazi kikuu. Ishara ya kwamba kiima cha kishazi kikuu hakiathiri upatanisho wa kishazi nomino hiki. Hebu tutazame kielelezo cha kifuatacho cha sentensi 25b.

27. a) Shiraz amesema atakupigia simu.



b) atakupigia simu*




Katika vielelezo hivi, tunaona kwamba upatanisho wa kiambishi cha kiima katika kishazi kikuu na kishazi nomino 'kwamba' ni sawa hasa kwa sababu kiima cha kishazi kikuu ndicho kinachoathiri upatanisho huu. Kama tunavyoona katika kishazi nomino 'kwamba', hakuna kiima kilichobainika wazi. Kwa hivyo, tunachukulia kwamba kiima cha kishazi nomino 'kwamba' ni sawa na kiima cha kishazi kikuu ambacho ni *Shiraz.*

Katika nafasi ya kijalizo cha kiima, kishazi nomino hakiathiriwi na upatanisho wa kiima cha kishazi kikuu. Mathalan:

28. Alilomwambia ni [kwamba utakuja kujuta.]

Upatanisho uliopo ni ule unaopatikana katika kishazi nomino chenyewe. Hakuna athari kutoka nje. Hali hii pia inadhihirika katika matumizi ya kishazi nomino 'kwamba' katika nafasi ya kijalizo cha jina. Kwa mfano:

29. Tuna furaha [kwamba mmeweza kufika katika arusi yetu].

## 4.5 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeichunguza ruwaza ya upatanisho wa kishazi kikuu na kishazi nomino cha Kiswahili Sanifu. Kutokana na data tuliyotumia tumeweza kubainisha ya kwamba kishazi kikuu na kishazi nomino huathiriana kiupatanishi. Tumebainisha pia kwamba athari hii hutegemea nafasi za kisintaksia zinazochukuliwa na kishazi nomino.

# SURA YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

Tangu mwanzoni mwa utafiti huu, tumekuwa tukijadili vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu. Tumeweza kuviainisha katika kategoria tatu kimuundo:

a) kishazi nomino rejeshi

b) kishazi nomino kisoukomo

c) kishazi nomino 'kwamba'

Baadaye tulitathmini nafasi za kisarufi zinazochukuliwa na vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu. Tuliweza kubainisha kwamba vitenzi vya Kiswahili Sanifu huweza kuamua nafasi mbalimbali za agiumenti kama vile mtenda, mtendwa, mtendewa, mwathiriwa na mrejelewa. Nafasi hizi huchukuliwa na KN. Tuliweza pia kubainisha kwamba nafasi za agiumenti zinazoamuliwa na kitenzi cha Kiswahili Sanifu zinalingana kimuundo na nafasi za kisintaksia kiima, yambwa tendwa na yambwa tendewa. Pia tulizitambua nafasi zingine za kisintaksia ambazo haziwezi kuwa za agiumenti kwani haziamuliwi na kitenzi cha Kiswahili Sanifu. Nafasi za agiumenti tuliona kwamba huchukuliwa tu na KN na mara nyingine kishazi nomino. Kishazi nomino ambacho huchukua nafasi za agiumenti ni kishazi nomino rejeshi ambacho huchukua nafasi ya mtenda, mwathiriwa, mtendwa na mtendewa. Nafasi ya mrejelewa ndiyo nafasi ya pekee ya agiumenti tuliyoweza kubainisha kuwa huchukuliwa na vishazi nomino vyote vitatu bila kukosa usarufi. Hii ni kwa sababu agiumenti katika nafasi hii zaweza kuwa ni halisi au za dhahania. Hii ni kinyume na nafasi zingine tulizoorodhesha awali ambazo huchukua agiumenti halisi na hivyo huweza kuchukua kishazi nomino rejeshi tu. Kishazi nomino rejeshi kimetajwa na

wasomi kama vile Quirk na wengine (1972) na Biber na wengine (1999) kama kishazi nomino cha pekee kinachokaribiana zaidi na KN. Madai haya tumeyathibitisha katika utafiti wetu kwa kuthibitisha kwamba ni kishazi nomino rejeshi tu kinachoweza kutumiwa kwa utoano na KN katika sentensi. Isitoshe, tumeweza kubainisha kwamba vishazi nomino visoukomo na vya 'kwamba' huchukua nafasi zisizo za agiumenti. Kishazi nomino rejeshi pia huchukua baadhi ya nafasi zisizo za agiumenti.

Ikumbukwe kwamba kishazi nomino kisoukomo na kishazi nomino 'kwamba' huweza pia kuainishwa kama vishazi jalizi kwa sababu ya sifa yao ya kutumika kama vijalizi. Kwa hivyo, tunaona kwamba vishazi hivi vinabanika kimatumizi kuliko kishazi nomino rejeshi. Kwa jumla tunaweza kusema kwamba kutokana na utafiti wetu, tumeweza kuthibitisha kwamba vishazi nomino vina uamilifu sawa na wa virai nomino ila havina uhuru mwingi kama wa virai nomino hasa kutokana na muundo na matumizi yake.

Utafiti huu pia ulijaribu kuchunguza ruwaza ya upatanisho baina ya kishazi kikuu na kishazi nomino. Tulichunguza jinsi kishazi kikuu kinavyoathiri au kinavyoathiriwa na kishazi nomino kiupatanishi. Kutokana na data tuliyotumia, tuliweza kubainisha kwamba kutegemea nafasi zinazochukuliwa na kishazi nomino katika sentensi, kishazi kikuu kinaweza ama kuathiri au kisiathiri upatanisho wa kishazi nomino. Tumedhihirisha kwamba kishazi nomino rejeshi huathiriwa na kishazi kikuu kinapotokea katika nafasi ya yambwa tendwa au yambwa tendewa. Pia kishazi nomino rejeshi huathiri kishazi kikuu kinapotokea katika nafasi ya kiima. Kishazi nomino kisoukomo pia katika nafasi ya kiima huathiri upatanisho wa kishazi kikuu. Hata hivyo, kinapotokea katika nafasi

zingine, kishazi nomino hakiathiriwi na kishazi kikuu kiupatanisho. Kishazi nomino 'kwamba' hakiathiriwi wala kuathiri upatanisho wa kishazi kikuu kinapotokea katika nafasi ya kijalizo. Hata hivyo, katika nafasi ya yambwa, kishazi nomino 'kwamba' huelekea kuathiriwa kwa kiasi fulani na kishazi kikuu. Kwa jumla, tunaweza kusema kuwa kishazi kikuu na kishazi nomino hutegemeana kiupatanishi kutegemea nafasi inayochukuliwa na aina mbalimbali za vishazi nomino vya Kiswahili Sanifu.

Katika jaribio letu la kubainisha kama nadharia ya uminimalisti inafaa katika uchanganuzi wa sentensi changamano za Kiswahili Sanifu, tumeweza kubainisha kwamba inaelekea kwamba nadharia hii inajikita sana katika ufafanuzi wa sentensi sahili na kwa sababu hii tunaona kwamba habari za sentensi zinabebwa na kitenzi kikuu katika sentensi. Vitenzi vingine ambavyo vinatokea katika sentensi kama vitenzi tegemezi haviwezi kuchanganuliwa katika mchoro mmoja. Inabidi vichanganuliwe katika mchoro tofauti. Jambo hili linaelekea kutenganisha habari ambazo zinaunganishwa katika sentensi changamano na hivyo kuleta utata katika uchanganuzi. Ikumbukwe kwamba katika lugha asilia, sentensi changamano na ambatani hutumiwa kwa wingi katika mawasiliano. Ni maoni yetu kwamba kuwepo kwa nadharia inayoweza kuchanganua sentensi hizi bila kuzitenganisha itakuwa imepiga hatua kubwa katika uchanganuzi wa lugha asilia za kilimwengu.

## 5.1 MAPENDEKEZO

Katika kuufanya utafiti huu tumekumbana na changamoto mbalimbali ambazo baadhi yake tumejaribu kutatua na nyingine hatukuweza hasa kwa sababu ya kujikita katika

mipaka ya utafiti huu. Kutokana na changamoto hizi, tungependa kupendekeza kwamba tafiti zaidi zifanywe katika kuchanganua vishazi vingine tegemezi vya Kiswahili Sanifu kama vile vishazi elezi na vishazi linganishi. Tumejaribu kuelezea muundo wa agiumenti wa kitenzi cha Kiswahili Sanifu. Hata hivyo, maelezo yetu yamejibana katika upeo na mipaka ya utafiti wetu. Tunaonelea kwamba utafiti wa kina unahitajika katika eneo hili ili kuweza kuchangia katika tafiti zinazogusia masuala ya agiumenti.

# MAREJELEO


Abdulaziz, M.H. (1996) *Transitivity in Swahili* Koln: Ruediger Koeppe Verlag

Ashton E.O. (1944) *Swahili Grammar:Including Intonation* London: Longman

Baker M.C. (2003) *Lexical Categories: Verbs, Nouns and Adjectives* Cambridge: Cambridge University Press

Biber na wenzake (1999) *Longman Grammmar of Spoken and Written English* London: Longman

Bussmann H. (1996) *Routledge Dictionary of Language and Linguistics* London: Routledge Reference

Chomsky, N (1957) *Syntactic Structures* Moulton: The Hague

_________ (1965) *Aspects of the Theory of Syntax* Massachussetts: Cambridge University Press

________ (1995) *The Minimalist Program* Cambridge: MIT Press

Cook V.J. & M. Newson (1988) *Chomsky's Universal Grammar 2nd Edition: An Introduction* Oxford: Blackwell

Cristofaro S. (1990) *Subordination* Oxford: Oxford Uiversity Press

Crystal, D. (2003) A Dictionary of Linguistics and Phonetics 5th Ed. Oxford: Blackwell

DeCarrico J.S. (2000) *The Structure of English: Studies in Form and Function for Language Teaching.* USA: The Michigan University Press

Grimshaw J. (1990) *Argument Structure* Massachusetts: Massachusetts Institute of Technology

Habwe J. na P. Karanja (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili* Nairobi: Phoenix Publishers

Hadumond B. (1996) *Routledge Dictionary of Language and Linguistics* London: Routledge Reference

Haegmann Lilliane (1994) *Introduction to Government & Binding Theory 2nd Edition* Oxford: Blackwell Publishers

Hornstein N. (1995) *Logical Form: From GB to Minimalism* Cambridge: Blackwell

Horrocks G. (1987) *Generative Grammar* UK: Longman Ltd

Huddleston R. (1984) *Introduction to the Grammar of English* Cambridge: Cambridge University Press

Jerono P. (2005) *Kishazi Huru Arifu cha Kiswahili* Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Kapinga A. (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* Dar es Salaam: TUKI

Kaviti L. (2004) *A Minimalist Perspective of the Principles and Parameters in Kikamba Morphosyntax* Tasnifu ya PhD Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Leech G. & J. Svartik (2000) *A Communicative Grammar of English 2nd Edition* London: Longman

Loogman A. (1965) *Swahili Grammar & Syntax* Pittsburgh: Duquesne University Press

Massamba D.P.B. et al (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu:Sekondari na Vyuo* Dar es Salaam: TUKI

Mdee J.S. (1986) *Kiswahili Muundo na Matumizi Yake* Nairobi: Intercontinental Publishers Ltd.

Mgullu R.S. (1990) *The Structure of Swahili Sentences: A Transformational Approach* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Mgullu R.S. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili* Nairobi: Longhorn Publishers

Mkude D. .J. (2005) Uchambuzi wa Sentensi za Kiswahili katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1* Dar es Salaam: TUKI

Mogambi H.M. (2001) *Upatanisho wa Kisarufi katika Sintaksia ya Kiswahili: Mtazamo wa Umiliku na Masharti* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Mohammed M.A. (2001) *Modern Swahili Grammar* Nairobi: East African Educational Publishers

Mutua J. N. (2005) *Kishazi Kitegemezi cha Kiswahili Sanifu: Mtazamo wa X-baa* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Myachina E.N. (1981) *The Swahili Language: A Desriptive Grammar* London: OUP

Oichoe P. (2005) *Ulinganishi wa Kirai Tenzi cha Kiswahili na Ekegusii Kimofosintaksia* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Olali T. M. (1997) *Kikundi Nomino cha Kiswahili: Mtazamo wa Sintaksia ya X-Bar* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Payne T.E. (1997) *Describing Morphosyntax: A guide for field linguists* Cambridge: cambridge University press

Polome E. (1967) *Swahili Language Handbook* Washington D.C.: Centre for Applied Linguistics

Quirk R. na wenzake(1972) *A Grammar of Contemporary English* London: Longman

Quirk R. & S. Greenbaum (1973) *A University Grammar of English* Sussex: Longman

Radford A. (1997a) *Syntactic Thoery and the Structure of English: A Minimalist Approach* Cambridge: Cambridge University Press

Radford A. (1997b) *Syntax, Minimalist Introduction* Cambridge: Cambridge University Press

Swaleh R. H. (2005) *Mofosintaksia ya Kishazi cha Kitikuu: Mtazamo wa Uminimalisti* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Schroeder H. (2002) *Word Order in Toposa: An Aspect of Multiple Feature-Checking* PhD thesis University of Nairobi (haijachapishwa)

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* Dar es Salaam: TUKI

TUKI (2006) *English-Swahili Dictionary 3rd Edition* Dar es Salaam: TUKI

Vitale A. (1981) *Swahili Syntax* Holland: Foris Piblications

Webelhuth G.(ed) (1995) *Government and Binding Theory and The Minimalist Program* Cambridge: Blackwell